**KASHFA YA WODI** Mabula akubali yaishe, aomba radhi bungeni
UKURASA 3

**DUNI** achambua matatu magumu hatosahau siasa, uchaguzi Zanzibar
UKURASA 3



**WAPIGA** simu ya dharura afya kisha kutukana
UKURASA 10


ama
ALHAMISI SEPTEMBA 5, 2024
AFYA NA MAZINGIRA

Ujue ukweli kuhusu chupa za plastiki za maji hazileti saratani
Ukurasa 12

MAAJABU KISUKARI CHA MBUNGE... Dk. Malima aligundua kwa simu, Janabi akaendeleza safarini
Ukurasa 13

TAKA ZINAPOGEUZWA MALIGHAFI...
Waingia kazini kutekeleza mbadala wa Rais, kuacha mkaa uliozoeleka
Darasa laanza nyumbani, kisha wajasiriamali wadogo
Elizabeth Zaya

Kinamama wakionyesha kwa vitendo, namna ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutwanga malighafi kwenye kinu. Hiyo ni baada ya kupata mafunzo, kutoka Asasi ya Sauti ya Jamii Kipunguni, Ukonga Dar es Salaam. PICHA: ELIZABETH ZAYA

Hadi sasa, asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo cha mvua au maji na kadri wanavyoendelea kukata miti, uwezekano wa kupata maji ya kutosha unabaki mdogo, mkombozi dhidi ya magumu hayo ni kutumia nishati mbadala na rafiki kwa mazingira, unaookoa mengi.

"Tunawafundisha teknolojia hii waione kwamba ni fursa, lakini wakati huohuo tunalinda mazingira na kuokoa misitu yetu kwa faida ya vizazi na vizazi na kuepusha magonjwa yanayotokana na matumizi ya mkaa ule."

Anasema kwamba, mafunzo ya kutengeneza nishati hiyo ya mkaa mbadala wamepewa na Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), ikiwa ji matokeo ya teknolojia mpya inayokinzana na ukataji miti hololela.

WALENGA NA YAO

Dorice Alfred ni mjasiriamali kutoka Kata ya Kivule, wilayani Ilala, anaeleza alivyonufaika katika ujasiriamali wake wa kupika uji na vitafunwa, mafunzo yamemsaidia pia kutunza fedha, tangu ajifunze kutengeneza mkaa unaotokana na taka, umeachana na mkaa wa miti.

Inaendelea Uk. 12

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Septemba 5, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581790
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKATILI WATOTO

**Polisi yawaonya waganga wa jadi**



UKURASA 2

# Janabi alivyonusuru mbunge na kisukari

**SIMU** ilibaini tatizo; alipozembea, akanaswa Hijja, kliniki ikaanzia kwa wake... Endelea Uk 13 & 14



## TANZANIA, ZAMBIA ZAWEKA MAMBO SAWA NA CHINA KUFUFUA TAZARA

UKURASA 2 & 19

Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, wakishuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano ya kuboresha reli ya TAZARA, jijini Beijing, China jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **MZIZE: MIMI NI HATARI ZAIDI NIKIANZIA BENCHI** UK 24

MAONI, KATUNI UK.6



Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu operesheni mbalimbali za kudhibiti uhalifu zinazoendelea kufanywa na jeshi hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Balozi aeleza fursa ziara ya Samia China

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Tanzania nchini China, Khamis Omar, amesema kuwa Mkutano wa Nne wa Ushirikiano wa China-Afrika (FOCAC) utaimarisha ushirikiano na una fursa nyingi kwa maendeleo ya Watanzania.

Katika mahojiano maalum na Kituo cha Televisheni cha China cha CGTN, yaliyofanyika jana kuhusu matarajio yake juu ya mkutano huo na manufaa ya moja kwa moja kwa Watanzania, alisema utaendeleza pale walipoishia mwaka 2021 huku sekta za miundombinu, kilimo cha kisasa na teknolojia vikiwa kipaumbele.

Rais Samia yupo nchini China kwa ziara ya siku tano kuanzia Septemba 2 hadi 6, mwaka huu na tayari amefanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais Xi Jinping, ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Balozi huyo alisema mjadala mkubwa ni kwenye uchumi, uhusiano kati ya watu, maendeleo,teknolojia masuala ya kimataifa, usalama na nishati safi.

"Tangu jukwaa hili lilipoanzishwa mwaka 2000, huu utakuwa mkutano wa nne wa FOCAC, na kila mtu ana matarajio makubwa kwa jukwaa hili, kwa sababu linakutanisha tena wakuu wa nchi na serikali kutoka Afrika na China, wanakutana na Rais Xi Jinping hapa.

Watakuwa wenyeji na kujadili ushirikiano kati ya Bara la Afrika na China," alisema Balozi Omar.

Alisema uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China umekuwapo tangu 1964, ikiwa ni miongo sita sasa ambao ulianza kwa kuwa na aina moja ya idiolojia sawa, imani sawa kuhakikisha uhuru wa nchi zote, mamlaka na umoja wa eneo, kujitolea kwetu dhidi ya ukoloni na ushirikiano.

"Uhusiano huo ulizidi kukua hadi kuwa uhusiano wa chama kwa chama, ushirikiano wa kiuchumi, uhusiano kati ya watu, na nyanja nyingine muhimu pia," alisema.

Alisema mwaka 2022 marais wa Tanzania na China walikubaliana kuimarisha uhusiano huo na kuwa wa kina zaidi kwa manufaa ya pande zote. "Kuna maeneo muhimu matatu au manne. Moja ni kuhusu maendeleo ya miundombinu, wakati mwingine tunapozungumzia China na Tanzania, jambo la kwanza linalokuja akilini mwangu kama mimi mzee ni reli ya TAZARA.

"Hii ilikuwa mwanzo wa ushirikiano mkubwa wa miundombinu. Na tunavyofahamu, miundombinu ni muhimu sana kwa kufungua uchumi wa nchi yoyote, kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, kuunganisha nchi na sehemu nyingine za dunia,"alisema.

Alisema eneo la pili litakuwa upande wa uzalishaji, China, hata wakati wa miaka ya 1960 hadi sasa, imekuwa ikisaidia Tanzania katika maeneo ya uzalishaji, kilimo, utengenezaji.

**"China imekuwa mshirika wetu mkuu wa kibiashara, naona kwa miaka minane au tisa iliyopita. China ndiyo nambari moja kama mshirika wa kibiashara na tunavyofahamu, biashara ni muhimu sana kwa ustawi,bila kusahau sekta ya utalii," alisema.**

Aidha, alisema kwa sasa kuna nguvu ya sekta binafsi pande zote mbili kwa kuwa kuna kampuni za Kichina zinazokuja Tanzania kwa ajili ya uwekezaji.

"China imekuwa mshirika wetu mkuu wa kibiashara, naona kwa miaka minane au tisa iliyopita. China ndiyo nambari moja kama mshirika wa kibiashara na tunavyofahamu, biashara ni muhimu sana kwa ustawi,bila kusahau sekta ya utalii," alisema.

Pia jana Rais Samia na Rais wa Zambia,Haikande Hichilema, wameshuhudia utiaji saini wa Hati za Makubaliano ya Uboreshaji wa Reli ya TAZARA.

Maeneo mengine ya kipaumbele kwenye mkutano huo ni uendelezaji wa miundombinu, kukuza uwekezaji, uendelezaji wa viwanda, kilimo cha kisasa, amani na usalama.

Aidha, Rais Samia anatarajia kuwa miongoni mwa wakuu wa nchi watakaohutubia ufunguzi wa mkutano wa FOCAC akizungumza kwa niaba ya ukanda wa Afrika Mashariki.

# Polisi yaonya waganga wa jadi matukio ubakaji, ulawiti

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limekutana na waganga wa tiba mbadala 80 na kuwaonya kuacha kufanya ramli chonganishi kwa kuwapa masharti wateja wao kuwa ili wafanikiwe kibiashara na kupata utajiri, wajihusishe na vitendo vya ubakaji na ulawiti wa watoto.

Kamanda wa Polisi Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati ya jeshi hilo katika kushughulikia matukio ya ukatili dhidi ya makundi hayo kwa mujibu wa sheria.

Muliro alisema juzi Jeshi la Polisi lilifanya kikao na waganga hao wanaojulikana kama wa tiba mbadala kwa lengo la kuwaelimisha kuacha kujihusisha au kufanya ramli chonganishi.

"Kuacha tabia ya kuwapa masharti baadhi ya wateja wao kuwa ili wafanikiwe katika biashara na kupata utajiri, lazima wafanye vitendo viovu vya kuwalawiti au kuwabaka watoto.

"Jeshi la Polisi limetoa tahadhari na kuwaonya vikali waganga wanaofanya hivyo kuwa watakaobainika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

Kuhusu kusimamia mifumo ya kisheria na utekelezaji wa taarifa ya Tume ya Haki Jinai, Kamanda Muliro alisema jeshi hilo limeendelea kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wa matukio mbalimbali ya kihalifu ambao baadhi yao wamepatikana na hatia na kuhukumiwa kwa kupewa adhabu.

"Jeshi la Polisi limekuwa likichukizwa sana na vitendo vya ubakaji na ulawiti na katika hatua hiyo, washtakiwa katika kesi 16 kuanzia za makosa ya kubaka na kulawiti zilizosikilizwa kati ya Julai hadi Agosti, mwaka huu, walihukumiwa adhabu za vifungo cha maisha jela akiwamo Boniphace Paul (24), mkazi wa Mbezi kwa Musuguri," alisema.

Kamanda Muliro alisema mshtakiwa mwingine, George Godfrey (21), mkazi wa Chanika, Dar es Salaam, alikamatwa eneo la Coco Beach na kufikishwa mahakamani kwa unyang'anyi wa kutumia silaha ambako baada ya shauri lake kusikilizwa, alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Katika hatua nyingine, Kamanda Muliro alisema Septemba 3, mwaka huu, saa 2:00 usiku, jeshi hilo lilipokea taarifa kutoka kwa raia wema kuwa maeneo ya Tanganyika Parkers, Kawe, kulikuwa na watu wawili waliokuwa na mapanga wakitishia na kuwapora wapita njia.

"Ufuatiliaji wa polisi ulifanyika haraka na kuwakuta watu hao, walipotaka kukamatwa walikaidi na kutoa mapanga kutaka kumdhuru mmoja wa askari, ambaye alijihami kwa kupiga risasi hewani.

"Baadaye alipokuwa katika hatari kubwa ya kudhuriwa, alimjeruhi kwa risasi mtuhumiwa mmoja, Festo Maricha (27), mkazi wa Mbezi Luis na mwenzake ambaye hakufahamika jina alikimbia. Mtuhumiwa amepelekwa Hospitali ya Mwananyamala kwa matibabu," alisema Muliro.

Kamanda Muliro alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa mbalimbali zitazosaidia mkakati wa kuzuia zaidi vitendo vya kihalifu ili Dar es Salaam iendelee kuwa salama.

## HABARI KITAIFA

# Duni achambua matatu magumu hatosahau siasa, uchaguzi Z'bar

**Na Rahma Suleima,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji, amesema amepitia mito, milima na mabonde ya kisiasa ambazo hatasahau maishani mwake, ikiwamo kushitakiwa kwa kosa la uhaini.

Duni aliyasema hayo jana katika hafla ya kutunukiwa zawadi na chama chake kutokana na utumishi wake na sasa amebaki kuwa mlezi na mshauri wa ACT Wazalendo.

Alisema baada ya kushtakiwa kwa uhaini na kuwekwa gerezani kwa miaka minne, alipoteza wazazi wake wawili akiwa huko bila kushuhudia maziko yao.

"Jambo kubwa ambalo limenipata ambalo nikilikumbuka huwa ninasikitika ni wakati wa kesi ya uhaini. Wakati tunapandishwa mahakamani pale Vuga, mzee wangu, yaani baba yangu mzazi, alikuja kuniona kwa lengo la kunisalimia.

"Lakini jambo la kusikitisha mzee wangu hakupewa ruhusa na alipigwa na mmoja wa askari na akaanguka, huku nikiwa ninashuhudia na wala sijamwona tena mpaka amefikwa na mauti. Sikuruhusiwa kwenda kumzika. Kwa kweli mengi yananisikitisha, lakini hili ni gumu sana," alisema.

Duni alitaja jambo lingine kuwa ni Wazanzibari imekuwa kama utamaduni kila miaka mitano kuuawa kwa sababu ya uchaguzi. Alisema kila anapopata nafasi ya kuonana na viongozi wa kitaifa bila hofu wala kuogopa, amekuwa wakiwaambia kuhusu suala hilo.

"Huwa nawaambia hivyo jamani hakuna njia nyingine yoyote isipokuwa kuuana? Wazanzibari haiwezekani kufanya uchaguzi ukawa salama? Hivi tumelaaniwa sisi Wazanzibari, maana duniani kote watu wanagombana lakini hufikia siku watu hurudi katika meza wakazungumza na humaliza tofauti zao," alisema.

Duni alisema anashangaa kuona kuna muafaka wa maridhiano inafanyika Zanzibar kwa ajili ya kumaliza tofauti zao, lakini kila inapofika kipindi cha Uchaguzi Mkuu, huwa yanajitokeza mauaji makubwa, jambo hilo limekuwa likimkereketa, licha ya kusema kuwa anaamini kuna siku mambo hayo yataisha.

Alisema ili kuondokana na janga hilo ni lazima kushikamana na kuondokana na siasa za chuki na uhasama ambapo Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume, alihakikisha kujenga umoja wa Wazanzibari na alifikia hatua ya kutukanwa kwa kuanzisha ndoa za makabila ili kuwaunganisha.

Jambo lingine ambalo hatalisahau, alisema ni baada ya kufariki dunia kwa mwanasiasa mkongwe ambaye alikuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad na chama kupita katika misukosuko mikubwa.

Misukosuko hiyo aliitaja kuwa ni pamoja na kumpata mrithi wake katika nafasi ya Makamu wa kwanza wa Rais na mrithi wa mwenyekiti wa chama na yote hayo walifanikisha.

Alitaja jambo lingine ni uchaguzi mkuu wa chama wa kupanga safu za uongozi. Katika mchakato huo, alisema alipigwa majungu,lakini alifanikisha kusimamia akiwa katika nafasi ya mwenyekiti na hatimaye safu kamili na imara ya uongozi ikapatikana.

Duni alikishukuru chama chake kwa kitendo walichokifanya jana cha kumpatia zawadi na kuendelea kumuenzi akiwa bado yuko hai kwa sababu ni bahati kubwa kwake ya kukirimiwa.

Alisema baadhi ya viongozi wenzake waliokuwa pamoja katika mapambano, washatangulia mbele ya haki na hawakupata bahati hiyo, hivyo anajiona mwenye bahati kubwa.

Hata hivyo, Duni alisema licha ya kushawishiwa kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) lakini hana mpango huo.

"Sijafikiria wala sijadhani na wale wanaodhani kwamba Babu Duni anakwenda CCM. Mie?"alisisitiza.

# Mabula aomba radhi madai wagonjwa kulala wodi moja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Ilemela (CCM), Dk. Angelina Mabula, ameomba radhi bungeni na kufuta maneno yake kwamba wagonjwa wanaume, wanawake na watoto wanalazwa kwenye wodi moja katika Kituo cha Afya Sangabuye mkoani Mwanza.

Mabula amefikia hatua hiyo baada ya ushahidi wake aliowasilisha bungeni kuonesha kuwa jambo alilolisema si la kweli licha ya kituo hicho kukabiliwa na uhaba wa miundombinu.

Waziri huyo wa zamani wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, aliomba radhi juzi bungeni kabla ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kuahirisha kikao cha Bunge.

"Asante Mheshimiwa Spika (Dk Tulia Ackson) kwa kunipa fursa kusema maneno machache baada ya kutoa maelezo namna ulivyopitia ushahidi wote ulioletwa. Pamoja na maelezo uliosema utambuzi ni kwamba bado pana changamoto na bado pale wamezungumzia wanapozidi bado wanaingia kule.

"Kwa hiyo kama ilileta mtafaruku kwa namna ambavyo hali halisi nilivyoiwasilisha, Mheshimiwa Spika naomba kufuta hayo maneno lakini changamoto inabaki ile ile ya kwamba hakuna miundombinu na naomba radhi kama limeleta mtafaruku katika kuelewa hoja halisi niliyokuwa nimeileta," alisema Mabula.

Awali, Spika Tulia alisema: "Mtakumbuka Agosti 27, 2024 wakati wa maswali na majibu, Mheshimiwa Mabula alipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza na aliuliza Kituo cha Afya cha Sangabuye kilipandishwa hadhi 1999 kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya. Kituo hicho hadi leo kina wodi moja ambayo inatumika na wanawake, wanaume na watoto na kuhoji serikali lini itakamilisha miundombinu ikiwa ni pamoja na kujenga uzio."

Naibu Waziri Dugange alisema hilo jambo katika hali ya kawaida haliruhusiwi na kuahidi kufuatilia ili kujua nini kinachoendelea huko.

Kutokana na uzito wa jambo hilo, Spika huyo alielekeza Naibu Waziri Dugange akimaliza kujibu maswali, aende kufuatilia jambo hilo na kumpa taarifa.

Kwa mujibu wa Spika Tulia, kabla ya kuahirisha Bunge, Naibu Waziri huyo aliwasilisha ushahidi wa maelezo na picha ya hali halisi ya kituo hicho na alimpa taarifa mbunge kuhusu maelezo hayo ya serikali ambayo yalibainisha kuwa kituo hakina wodi lakini watumishi wamejiongeza wameweka sehemu tatu za kulaza wagonjwa.

"Ile taarifa ilionesha kuwa wodi hakuna isipokuwa vyumba ambavyo vingetumika kwa ajili ya shughuli nyingine hapo vinatumika kwa ajili hiyo wakati wa kusubiri ujenzi wa wodi. Mheshimiwa Mabula alisimama na kuomba mwongozo kuwa yale maelezo yaliyotolewa kama ushahidi hakuna uhalisia kwa kuwa yeye amefanya ziara kwenye hilo eneo hivi karibuni na kukuta wanawake, wanaume na watoto wanalala sehemu moja," alisema.

Spika Tulia alisema alimhoji mbunge huyo kama ushahidi uliotolewa ni uongo na alisimamia msimamo wake kuwa maelezo aliyotoa ndio uhalisia ulioko kituoni hapo na kumtaka awasilishe Ushahidi unaothibitisha jambo hilo.

Alisema katika kuchambua ushahidi alichosema mbunge, kituo cha afya kina changamoto ya miundombinu ni kweli lakini hoja ya wagonjwa kulala pamoja si kweli.


## UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM

### INVITATION FOR BIDS

### INVITATION FOR BID FOR SUPPLY OF FIELD VEHICLES

**Date: September 2, 2024**

1. Ujamaa-Community Resource Team (UCRT) is a non-profit environmental and social justice organization, which works with tradition groups of different cultures. The target communities are those who depend on communal resource management regimes to support their livelihood. UCRT has set aside funds to be used to cover eligible payments for the supply of field vehicles and now invites sealed bids from eligible bidders for pre-qualification for the supply of field vehicles.
2. The bid will be opened in public on Friday, September 13th , 2024, at 16:00 pm (in the Ujamaa Community Resource Team general office) in the presence of the bidders or their fully appointed representatives who may attend. Bids not received and opened in public at the bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation, irrespective of circumstances.
3. The UCRT Procurement Committee is not bound to accept the lowest bid.
4. Bids not received before the deadline will not be accepted for evaluation irrespective of circumstances.
5. Interested applicants may obtain further information by contacting through Email: **procurement_ucrt@ujamaa-crt.or.tz** copying to **info@ujamaa-crt.or.tz**, from 08:00-15:30 on Mondays to Fridays except on public holidays and weekends.
6. All bids should be delivered in a **SEALED** envelope and Marked **SUPPLY OF FIELD VEHICLES**
7. The payment terms: Payment of 50% on signing the agreement and a final payment of 50% up on delivery and handover of vehicle to Ujamaa Community Resource Team at Arusha office.
8. The deadline for submission of bids will be 15:00 pm, September 13, 2024 local time
9. **Evaluation criteria**

| S/N | Description | Information to be submitted | Relative importance |
|---|---|---|---|
| 1. | Administrative and Legal documents | ▪ Certificate of incorporation or registration<br>▪ Current tax clearance certificate<br>▪ Proof of using EFD machine<br>▪ TIN number and VAT certificate (If applicable)<br>▪ Anti-bribery and Corruption policy | Comply/not comply |
| **2.** | **Technician** | | |
| 2 (a) | Warrant conditions | Indicate the terms and conditions. for the applications of Warranty | 5% |
| 2 (b) | Vehicle delivery time | Consideration will be given to prompt delivery of vehicles | 15% |
| 2 (c) | Vehicle characteristics | Availability of spare parts, New brand , manual, right-hand drive and white color | 20% |
| **3.** | **Financial** | | |
| 3(a) | Price | Prepare quotation for Vehicle -The total price/cost for the Vehicle MUST include taxes and other costs-quoted in USD, and TZS equivalents. | 60% |

**Note:** UCRT is committed to the highest ethical standards of transparency, openness, and accountability in its affairs. UCRT promotes a "zero tolerance" policy toward fraud and corruption. All communications should be channeled to the official correspondence email provided below:

**Procurement Committee**
**Ujamaa Community Resource Team,**
**P.O.BOX 15111, Arusha**
**Email: procurement_ucrt@ujamaa-crt.or.tz**

# Uwekezaji wahudumu afya ngazi jamii kupunguza mzigo

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI wa Huduma za Kinga na Elimu ya Afya Zanzibar, Dk. Salim Slim, amesema uwekezaji unaofanywa na serikali kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, utasaidia kupunguza mzigo mkubwa wa upungufu wa matumizi ya tiba kwa hospitali za juu na rufani.

Pia amesema wahudumu hao watasaidia kutoa elimu ya lishe chini na kutatua tatizo hilo ambalo bado lipo nchini.

Dk. Slim aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua kikao kazi cha nne kilicholenga kuandaa mpango kabambe wa kitaalamu ili kuwezesha utekelezaji Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii.

Kikao hicho kimeandaliwa na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Barani Afrika (Africa CDC) pamoja na Wizara ya Afya na kujumuisha wadau watekelezaji na wafadhili mbalimbali wanaofanya kazi katika eneo la afya ya jamii.

Dk. Slim alisema mada kuu ya kikao hicho ni kuzungumzia uratibu wa masuala ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

"Nchi zenye kipato cha chini na kati, tuna uhaba wa wafanyakazi ambao ni nesi na madaktari na papohapo, kuna wananchi wako nyumbani wanashindwa kuja vituoni kupata huduma kutokana na matatizo ya kifedha au utashi wa mtu," alisema.

Dk. Slim alisema kuwekeza katika kundi hilo kutabadilisha mwenendo wa utoaji huduma na ndio maana ni lazima kuwafundisha, kuwawezesha na kuhakikisha wanapata stahiki nzuri ili wasaidie.

Alisema wahudumu hao watasaidia katika eneo la chanjo kupitia malengo ambayo serikali zote mbili ambayo zimejiwekea, kuhakikisha maradhi yote yanayoweza kuondoka kwa chanjo yanaondolewa. Ofisa kutoka Wizara ya Afya, Mpango wa Taifa wa Huduma za Afya Ngazi ya Jamii, Dk. Meshack Chinyuli, alisema kuwa Januari 31 mwaka huu, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alizindua mpango jumuishi wa kutumia wahudumu ngazi ya jamii.

Alisema baada ya uzinduzi, wizara hiyo, TAMISEMI walianza utekelezaji.

"Mpango huo unatarajia kuweka zaidi ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 137,000, ambapo kila kijiji na tunakwenda hadi ngazi ya kitongoji kitapata wahudumu wa ngazi ya jamii wawili. Kwa upande wa mjini kila mtaa nako watakuwa na wahudumu hao wawili," alisema.

> **"Nchi zenye kipato cha chini na kati, tuna uhaba wa wafanyakazi ambao ni nesi na madaktari na papohapo, kuna wananchi wako nyumbani wanashindwa kuja vituoni kupata huduma kutokana na matatizo ya kifedha au utashi wa mtu," alisema.**

Mtaalamu wa Afya Jamii kutoka Africa CDC, Addis Ababa, Ethiopia, Dk. Barnabas Yeboah, alisema wanachofanya ni kusaidia nchi wanachama kama Tanzania, ili kuimarisha mifumo yake ya afya na kujiandaa kutambua, kulinda na kukabiliana na milipuko ya magonjwa yoyote.

Alisema wanafanya kazi na nchi ili kuhakikisha wanaweza kuajiri, kutoa mafunzo na kupeleka wahudumu wa afya katika jamii, kusaidia katika kuzuia na kudhibiti magonjwa.

Meneja wa Afya Kitengo cha Afya Msingi, UNICEF, Ofisi ya Tanzania, Dk. Ulrika Baker, alisema wana ushirikiano mkubwa na Wizara za Afya za Tanzania, Bara na Zanzibar katika kuimarisha huduma za afya ya msingi.

# Sharti la lazima kuonesha bei za bidhaa laondolewa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani kwa Mwaka 2024 umepitishwa na Bunge huku likifuta kifungu chenye sharti la lazima la wauzaji bidhaa au huduma kuonesha bei ya kila bidhaa au huduma na kuweka adhabu ya faini isiyopungua Sh. 10,000 na isiyozidi Sh. milioni moja ili kulinda walaji.

Hatua hiyo ilifikiwa baada ya ushauri wa wabunge, ikiwamo kukosa tafsiri ya mfanyabiashara mdogo na hivyo Bunge kushauri kifungu hicho cha 17 kilichoandikwa upya kuweka sharti hilo, kitumike kifungu cha awali kwenye Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2023 ambacho hakina sharti la lazima.

Akifafanua nje ya Bunge baada ya kupitishwa Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, alisema muswada huo ulikuwa na vifungu 24 na hivyo Bunge limepitisha vifungu 23 na hicho kimoja serikali imepewa muda zaidi wa kufanya utafiti na kutafuta tafsiri ya baadhi ya maneno ambayo yataleta utata kwenye utekelezaji wake.

Waziri Jafo alisema kuwa suala la kuweka bei za bidhaa, Bunge limeshauri kitumike kifungu cha awali na kutumia utaratibu wa mwanzo bila kuweka adhabu na ikiwezekana yafanyike maboresho kwa lengo la kutekeleza sheria kwa ufasaha na wafanyabiashara kuzingatia matakwa ya sheria inavyotaka.

"Mjadala umekuwa mzuri, tumekuwa na Muswada wa Sheria ya Tume ya Ushindani (FCC) ambao lengo lake lilikuwa kumjali mteja hasa upande wa wamiliki wa hodhi wa soko kutoka asilimia 35 hadi 40," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Erio, alisema sheria hiyo ni ya muda mrefu na kwamba marekebisho hayo yatawawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kufikia malengo ya serikali ya kuvutia biashara na kumlinda mtumiaji bidhaa au huduma. "Marekebisho yaliyofanyika ni mengi, ikiwamo kubadilisha vifungu vya ushindani na kuruhusu tume kutoa adhabu katika makosa yanayomwathiri mlaji ambapo vifungu vingine havikuwapo mwanzo, tunashukuru serikali kwa maboresho haya, yakianza kutumika tutatoa elimu ili watu waelewe zaidi," alisema. Juzi wakati wa mjadala bungeni kuhusu muswada huo, wabunge walishauri kifungu hicho kifutwe kwa kuwa kitaumiza wafanyabiashara wadogo, hasa machinga na mama na baba lishe na kushauri kiangaliwe upya.





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA MARA, SIMIYU NA MANYARA (BABATI DC, HANANG DC, MBULU DC NA BABATI TC)**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa nne utafanyika katika Mikoa ya Mara, Simiyu, na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati tarehe 04 hadi 10 Septemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 04 hadi Jumanne tarehe 10 Septemba, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***
**Limetolewa tarehe 27 Agosti, 2024 na:**

Juma Rahisi.
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI

HABARI KITAIFA

# Madereva wafunga barabara kushinikiza NEMC iwape vibali

Na Grace Mwakalinga

MADEREVA 150 wa malori yanayosafirisha vyuma chakavu kutoka Malawi kwenda Uganda na Rwanda, wamefunga kwa muda barabara ya Mpaka wa Kasumulu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya wakishinikiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutoa vibali vya kusafirisha vyuma hivyo.

Imedaiwa kuwa kwa zaidi ya mwezi mmoja, madereva wa magari hayo wamezuiwa kuendelea na safari katika mpaka huo baada ya NEMC kudai hawana vibali vya kusafirisha bidhaa hiyo.

Dereva Omary Salmini alisema wameshangazwa na uamuzi wa NEMC kuwazuia kuendelea na safari kwa madai ya kusubiri kupata kibali cha kusafirisha vyuma hivyo kwenda nchi za Uganda na Rwanda.

Alisema kuwa kwa muda wote wamekuwa wanasafirisha bidhaa hiyo kwa kutumia mpaka huo bila vikwazo, lakini wanashangazwa na katazo la sasa kwamba wasubirie vibali; wamekaa mpakani kwa zaidi ya mwezi mmoja "na hakuna cha maana kinachoendelea".

Alisema: "Tangu Agosti Mosi mwaka huu tumepaki magari yetu hapa baada ya kuzuiwa na NEMC hadi tuwe na vibali vya kusafirishia vyuma chakavu.

"Maisha yetu yamekuwa magumu kwa sababu hatuna fedha za kuendelea kujikimu, tumeacha familia huko zinatutegemea, usalama wa afya zetu uko hatarini kwa sababu mazingira si rafiki," alilalama Salmini.

Abdumalick Kanoti alisema utoaji vibali ulipaswa kufanywa ndani ya muda mfupi, lakini zoezi linasuasua kwa sababu NEMC hawana ofisi katika mpaka huo wala ofisa anayeshughulikia suala hilo kwa haraka.

"Tunaomba mamlaka zitusaidie suala hili, tunahitaji tuendelee na safari, tumechoka kukaa hapa kila siku tunapigwa kalenda, maisha yamekuwa magumu, hatuna fedha za kujikimu," alisema Kanoti.

Aliongeza magari na madereva wanaosafirisha vyuma hivyo kwenda nchi za Uganda na Rwanda, wengi wao ni Watanzania, hivyo kuendelea kuzuiwa katika mpaka huo ni kukosesha serikali mapato.

Mkurugenzi wa NEMC Kanda ya Mbeya, Josiah Murunya, alipotafutwa na Nipashe juzi, alisema suala hilo wanalifanyia kazi na kuahidi utaratibu wa vibali ukikamilika, madereva hao wataendelea na safari.

Jana, mwandishi wa habari hii alimtafuta tena Mkurugenzi Murunya ambaye alisema wamiliki wa magari ya kusafirishia vyuma chakavu kutoka Malawi kwenda Uganda na Rwanda kupitia Mpaka wa Kasumulu walipaswa kushughulikia vibali vya kusafirisha bidhaa hiyo Malawi kabla ya kuingia Tanzania.

Alisema mchakato wa kupata vibali ulipaswa kushughulikiwa kabla ya magari hayo kuingia nchini ili kuondokana na adha ya kuzuiwa kuendelea na safari kwa kuwa kutokuwa na vibali vya kusafirisha bidhaa hiyo ni tatizo.

"NEMC tulizuia magari hayo kuendelea na safari kwa sababu madereva hawakuomba vibali ya kusafirisha vyuma chakavu nchini Malawi ambako walichukua bidhaa hiyo.

"Walipaswa kupewa nyaraka ambazo zimetiwa saini na Serikali ya Malawi pamoja na Tanzania ndipo waruhusiwe kuingia nchini," alisema Muruya.

Aliongeza kuwa NEMC inaendelea kushughulikia suala hilo, ikiwamo kufanya mkutano na madereva hao kuhakikisha wanakamilisha utaratibu wa vibali kisha waendelee na safari kwenda nchi walizokusudia.

# Wacomoro kutibiwa Benjamin Mkapa

## -Spika wao akoshwa uwekezaji mkubwa

Na Ludovick Kazoka, DODOMA

RAIA wa visiwa vya Comoro sasa watatibiwa Tanzania kwa huduma walizokuwa wakizifuata Ulaya na Mashariki ya Mbali.

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Visiwa vya Comoro, Moustadroine Abdou, akiongea na waandishi wa habari jijini hapa jana, alisema wananchi wa Comoro hawana haja ya kusafiri mpaka Ulaya na Mashariki ya Mbali kufuata huduma za afya.

"Huduma tulizokuwa tunazifata Ulaya na Asia kama upandikizaji figo kumbe tunaweza kuzipata hapa Tanzania," alisema Spika huyo wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro alipotembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH).

Spika Abdou alitembelea Idara za Magonjwa ya Moyo, Huduma ya Upandikizaji Uloto (Tiba ya Sikoseli), Idara ya Radiolojia (MRI), Kliniki Maalum ya Viongozi na Wodi ya Rais katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema ziara hiyo imempa fursa Spika wa Bunge wa Visiwa vya Comoro kushuhudia mageuzi makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Tanzania katika sekta ya afya.

> **"Pia ameona mradi wa Kituo cha Nuclear Medicine cha BMH ambao umefikia asilimia 50. Kituo hiki kitakuwa ni Kituo cha Umahiri wa Matibabu ya Saratani katika Afrika.**

"Pia ameona mradi wa Kituo cha Nuclear Medicine cha BMH ambao umefikia asilimia 50. Kituo hiki kitakuwa ni Kituo cha Umahiri wa Matibabu ya Saratani katika Afrika.

"Tutashirikiana na Chuo Kikuu cha Havard cha Marekani," alisema Naibu Waziri Mollel. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Dk. Kessy Shija, alisema hospitali hiyo inatoa huduma kwa zaidi ya wananchi milioni 14 katika Kanda ya Kati na mikoa ya jirani.

"BMH tunatoa huduma za afya za ubingwa wa kati na ubingwa wa juu kama upandikizaji figo na upandikizaji uloto ambayo ni tiba ya sikoseli," alisema Dk. Shija kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Prof. Abel Makubi.

Dk. Shija aliongeza kuwa katika ushirikiano huo wa BMH na Visiwa vya Comoro, hospitali hiyo itafanya huduma mkoba (medical outreach) katika visiwa hivyo vilivyoko kusini mashariki mwa Bara la Afrika.

"Ushirikiano pia utahusisha mafunzo kwa wataalamu kutoka Comoro kuja kufanya mafunzo ya vitendo hapa BMH," alisema Dk. Shija.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kushoto), akimsikiliza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, walipofanya mazungumzo ofisini kwake, Ilala Boma jijini humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Chalamila, Kamishna Mkuu TRA wateta

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amekutana na kufanya mazungumzo na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda.

Katika kikao hicho kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliyoko, Ilala Boma jijini, Kamishna Mkuu Mwenda aliongozana na baadhi ya wataalamu wa mamlaka hiyo.

Chalamila, pamoja na mambo mengine, alizungumzia mambo kadhaa yaliyojadiliwa ikiwa ni kupunguza migogoro ya kikodi inayolalamikiwa na wafanyabiashara na kutanua wigo wa walipakodi kulingana na vyanzo vingi vya mapato vilivyomo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mkuu wa Mkoa, Chalamila pia alisema wamezungumzia kuboresha miundombinu ya kikodi ili TRA ikusanye mapato zaidi.

Kwa upande wake Kamishna Mkuu Mwenda alimshukuru Chalamila kwa ushirikiano anaotoa kwa kufanya kazi na TRA katika wilaya zote tano za Dar es Salaam na kuthibitisha kuwa mkoa huo ni kitovu cha biashara kwa kuwa unakusanya kodi zake zote kwa takribani asilimia 80.

Mkuu wa Mkoa Chalamila alipongeza TRA kwa jitihada mbalimbali inazochukua kutanua wigo wa kodi na kuahidi ushirikiano na kuhakikisha kodi inakusanywa kwa maendeleo ya taifa.

Hivi karibuni Mkoa wa Dar es Salaam ulikumbwa na migomo ya wafanyabiashara katika baadhi ya masoko, yakiwamo Soko la Kimataifa Kariakoo na machinga wa eneo la Simu 2000, wilayani Ubungo, mgomo ambao baadaye ulichukua sura ya kitaifa, hata kusababisha kufanywa mabadiliko katika Baraza la Mawaziri.

Mkuu wa Mkoa Chalamila ni miongoni mwa watendaji wa serikali waliojitokeza hatua za awali kutatua mgogoro huo, akizungumza na wafanyabiashara walioitisha migomo Kariakoo na Simu 2000.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la miundombinu rafiki wenye ulemavu si mjadala

**TAASISI** za umma na binafsi nchini zimekuwa zikifanya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya sekta kadhaa kama vile elimu, afya, uchukuzi na usafirishaji na nyumba za makazi. Lengo la kujenga miundombinu hiyo ni kuwaondolea wananchi kero na kuleta ufanisi katika sekta mbalimbali kwa manufaa ya wadau na taifa kwa ujumla.

Katika ujenzi wa miundombinu hiyo kama vile barabara, hospitali na vituo vya afya, viwanja vya ndege, vituo vya mabasi, shule na vyuo, miongoni mwa mambo yanayosisitizwa ni kuwapo kwa mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu. Katika ujenzi wa majengo kama hospitali na shule kwa mfano, kumekuwa na kasi ya ujenzi wa maghorofa jambo ambalo kama suala la wenye ulemavu halitazingatiwa, kuna hatari ya kundi hilo kupata matatizo wanapokwenda kupata huduma stahiki.

Hivi sasa kwa mfano, kumekuwa na kasi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo tayari imeshaanza kutoa huduma kati ya Dar es Salaam na Dodoma huku vipande vingine vya Makutopora hadi Tabora; Tabora hadi Mwanza na Mwanza hadi Isaka ujenzi wake ukiwa unaendelea. Mbali na ujenzi wa reli ya SGR, katika Mkoa wa Dar es Salaam, ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi unaendelea katika sehemu kadhaa.

Kuwapo kwa ujenzi wa miundombinu hiyo ya uchukuzi, kumeibua maswali kama suala la mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu hasa kwenye stesheni za SGR unazingatiwa.

Juzi, jijini Dodoma, wakati wa mkutano wa Bunge unaoendelea, Naibu Spika, Mussa Zungu, aliielekeza serikali kuchukua hatua za haraka kuimarisha huduma kwa watu wenye mahitaji maalum kwenye stesheni za reli ya mwendokasi. Zungu alitoa agizo hilo baada ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Asha Abdallah Juma, kuhoji lini serikali itaongeza idadi ya viti mwendo kwa ajili ya abiria wenye mahitaji maalum kwenye viwanja vya ndege na stesheni za SGR.

Kwa mujibu wa mbunge huyo, watu wenye mahitaji maalum wanapata shida sana kusafiri hasa kwenye stesheni za SGR kutokana na kutokuwapo kwa mazingira rafiki kwao, hususan kukosekana kwa viti mwendo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alisema serikali imeshapeleka viti mwendo vya umeme ambavyo vinasimamiwa na watoa huduma katika maeneo hayo. Pia, alisema watu hao wakiwamo madaktari kwenye viwanja vya ndege na stesheni za SGR wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya huduma hizo.

Licha ya Naibu Waziri kutoa majibu hayo, Naibu Spika huyo alielekeza hatua za haraka zichukuliwe ili kuimarisha huduma kwenye stesheni hizo ili watu wenye mahitaji maalum waondokane na adha wanayoipata. Kwa maagizo na maelekezo ya serikali katika mchakato wa ujenzi wa miundombinu, suala hilo limekuwa likisisitizwa na kwa sehemu kubwa linatakelezwa. Hivi sasa hakuna sehemu ambayo mtu anaweza kwenda na kukuta hakuna miundombinu ya kundi hilo la watu wenye ulemavu.

Pamoja na kuwapo huko, kama alivyohoji mbunge kuwa wenye ulemavu wanapata adha kutokana na kutokuwapo huduma toshelevu, ni vyema serikali ikajielekeza zaidi katika kutatua suala hilo. Mpaka mbunge kuhoji hivyo na naibu spika kutoa msisitizo, inawezekana kuna changamoto katika eneo hilo.

Jambo la msingi na la kuzingatiwa katika hilo ni kwamba mifumo ya miundombinu irekebishwe ili kuwawezesha wenye ulemavu kuondokana na adha ya kukumbana na vikwazo katika kupata huduma mbalimbali. Pia, katika miradi inayoendelea, taasisi maalumu za serikali zifuatilie takwa hilo la kuwapo kwa miundombinu ya watu wenye ulemavu.

Kwa kuwa ujenzi wa miundombinu ya kijamii na kiuchumi ni endelevu, taasisi zinazohusika na kazi hiyo, hazina budi kutambua kuwa jambo hilo si la kuibua mjadala bali kinachotakiwa ni utekelezaji pekee.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Beatrice Moses

# Kongole JWTZ, kweli mnapambana kwa ajili ya nafsi za wananchi

**JESHI** la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilianzishwa rasmi Septemba Mosi mwaka 1964, lengo likiwa kulinda uhuru wa nchi na mipaka ya Tanzania. Historia inaonesha tangu kuanzishwa kwake, imefanya mengi yakiwamo yanayoendelea kuweka kumbukumbu njema kwa wananchi.

Vyombo kadhaa vya habari vya ndani na nje ya nchi vimeripoti baadhi ya matukio hayo, yanayoonesha umahiri wa askari wa JWTZ, ikiwamo tukio la mwaka 1978, vita vya kumshikisha adabu Nduli Iddi Amini Dadah, aliyeichokoza Tanzania akitaka kumega ardhi ya Mkoa wa Kagera.

Aliyekuwa Rais wakati huo na Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Nyerere, hakumpa nafasi Nduli huyo kupata alichotamani, badala yake alimtangazia vita mchokozi Iddi Amini, akitamka Dadah: "Ametuchokoza; uwezo wa kumpiga tunao, sababu ya kumpiga tunayo, nia ya kumpiga tunayo, hivyo tumeamua kupambana naye."

Majeshi ya Tanzania yakiongozwa na JWTZ yalipambana na kushinda vita hiyo, Iddi Amini Dadah, baada ya kuelemewa alikimbilia nchini Libya kutafuta hifadhi. Ni wazi alishikishwa adabu hadi akaikimbia nchi yake.

Askari wa JWTZ wameshiriki kulinda amani kwenye nchi kadhaa barani Afrika miongoni mwao wapo wachache waliopata ulemavu, pia kadhaa walipoteza maisha yao, Mwenyezi Mungu awajalie pumziko la amani askari wa JWTZ waliopoteza maisha yao kwenye vita tofauti ikiwamo hiyo ya Uganda, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Liberia na Lebanon.

Askari hao, siyo mahiri kwenye vita pekee bali hata kwenye shughuli za kijamii wamekuwa wakijitokeza mstari wa mbele kama vile kwenye uchangiaji wa damu salama, shughuli za JWTZ limeadhimisha Siku ya Mazingira Juni 5 mwaka 2021, walifanya shughuli za utunzaji mazingira ikiwa ni pamoja na upandaji miti, kufanya usafi na michezo.

Walishiriki kwenye usafi mikoa tofaut,i ikiwamo mkoani Dodoma Soko la Ndugai, Hospitali ya Mkoa, Hospitali ya Makole mkoani Morogoro walisafisha Shule ya Msingi Mwenge iliyopo Kijiji cha Pangawe, Tabora, Hospitali ya Rufaa ya Kitete na wakati Dar es Salaam walifanya usafi, Hospitali ya Kigamboni, Shule ya Msingi Changanyikeni, Hospitali ya Vijibweni, na Barabara ya Tungi Ferry Kigamboni.

Pia, JWTZ imeshiriki katika matukio ya utoaji msaada wa uokoaji yanapotokea majanga, ikiwamo lililotokea mwishoni mwa Desemba mwaka 2023, katika maporomoko ya tope Kateshi Hanang mkoani Manyara, tarehe 26, mwezi uliopita katika maadhimisho ya miaka 60 tangu kuazishwa kwake limetoa huduma za matibabu bure kwa wananchi Nachingwea katika viwanja vya shule ya Msingi Majengo.

Matibabu yaliyotolewa hapo ni pamoja uchangiaji wa damu, wametoa huduma ya uchunguzi wa saratani ya matiti na shingo ya kizazi, saratani ya tezi dume kwa njia ya damu, upimaji wa homa ya Ini, kisukari, Kaswende, shinikizo la damu(BP), Upimaji wa VVU na uchunguzi wa kinywa na meno.

Ni wazi wananchi waliojitokeza kupata huduma hiyo, baadhi wamekaririwa wakielezea kufurahishwa na huduma hizo.

JWTZ, pia katika maadhimisho ya sherehe kadhaa za kimataifa wamekuwa wakishiriki na kuwavutia wengi hasa kwa maonyesho kadhaa ambayo hufanywa na askari wake ikiwamo wa kikosi cha Makomandoo, hivyo kwa namna fulani imekuwa ikitoa burudani ya aina yake ambayo hufurahisha hivyo kupunguza ama kuondoa msongo wa mawazo kwa baadhi ya wananchi.

Nimetaja matukio machache kati ya mengi yaliyofanywa na JWTZ, naamini yapo ambayo sitayataja kwa sababu ya nafasi kuwa dogo, lakini kwa hakika matendo wanayoonyesha umuhimu wa jeshi hilo kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Dhima ya JWTZ ni kulinda nchi na kutetea maslahi ya taifa la Tanzania, kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya kitaifa na kimataifa.

Majukumu yake ni kulinda Katiba na Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Ulinzi wa mipaka ya Tanzania;Kufanya mafunzo na mazoezi, kujiweka tayari kivita wakati wote; Kufundisha umma shughuli za ulinzi wa taifa.

Aidha, inashirikiana na mamlaka za kiraia kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji wakati wa maafa; kukuza elimu ya kujitegemea na uzalishaji kupitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT); na kushiriki katika ulinzi wa amani Kimataifa.

JWTZ ni mfano mzuri wa kuiga kwa namna wanavyomudu kutimiza majukumu yao na kujenga imani kwa wananchi, kwa hakika wameweza. Inatarajiwa kuendelea kuwa bora zaidi na zaidi, pongezi walizopewa hivi karibuni ikiwamo za kutoka kwa Rais Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan zinastahili kutokana na uwajibikaji wao .

TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

TAASISI YA KUTHIBITI UBORA WA MBEGU TANZANIA

TOSCI
TANZANIA OFFICIAL SEED CERTIFICATION INSTITUTE

## TAARIFA KWA UMMA

# UTOAJI WA RUZUKU YA MBEGU ZA MAHINDI ZILIZOTHIBITISHWA UBORA KATIKA MSIMU WA MWAKA 2024/2025

Tarehe: 2 SEP, 2024

1. Katika msimu wa 2024/2025, Serikali imepanga kutoa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora (certified seeds) katika mikoa yote yenye fursa ya uzalishaji wa zao hilo. Katika utekelezaji wa mpango huo, Wizara ya Kilimo imeiteua Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) kuratibu utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni pamoja na kusajili makampuni ya mbegu na mawakala watakaohusika katika mpango huu wa ruzuku ya mbegu za mahindi.

2. Katika kutekeleza jukumu hilo, TOSCI itatumia mfumo wa kidigiti ulioboreshwa ambao utajumuisha utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea. Aidha ili kupunguza mianya ya udanganyifu na kuimarisha usimamizi, mfumo huo pia utatumia programu maalum ya kidigiti ili kusajili wakulima, wazalishaji/waagizaji, wasambazaji na wauzaji wa mbegu hizo za mahindi.

3. Kwa msimu wa mwaka 2024/2025, bei kikomo ya ruzuku kwa aina mbalimbali za mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora itakuwa kama ifuatavyo:

| Kundi | | Na. | Aina ya mbegu | Uzito (Kilo) | Bei kikomo yenye ruzuku |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Aina za Mbegu zinazo-chavushwa huria (OPVs) | 1. | NATA K 60 | 2 | 7,000 |
| | | 2. | NATA K 8 | 2 | 7,000 |
| | | 3. | TZM 523 | 2 | 7,000 |
| | | 4. | LISHE K1 | 2 | 7,000 |
| | | 5. | Bora | 2 | 7,000 |
| | | 6. | TMV-2 | 2 | 7,000 |
| | | 7. | SITUKA M1 | 2 | 7,000 |
| | | 8. | Kilima | 2 | 7,000 |
| | | 9. | Staha | 2 | 7,000 |
| | | 10. | TMV - 1 | 2 | 7,000 |
| | | 11. | T105 | 2 | 7,000 |
| | | 12. | T104 | 2 | 7,000 |
| II | Aina za Mbegu chotara (Hybrid) zinazokomaa mapema na muda wa kati | 1. | NATA H 105 | 2 | 14,000 |
| | | 2. | UH 6303 | 2 | 14,000 |
| | | 3. | UH 615 | 2 | 14,000 |
| | | 4. | DK 8031 | 2 | 14,000 |
| | | 5. | DKC 80-33 | 2 | 14,000 |
| | | 6. | DKC 80-53 | 2 | 14,000 |
| | | 7. | SY 6444 | 2 | 14,000 |
| | | 8. | SY 5054 | 2 | 14,000 |
| | | 9. | PAN-3M-05 | 2 | 14,000 |
| | | 10. | 30G19 | 2 | 14,000 |
| | | 11. | P 3812 W | 2 | 14,000 |
| | | 12. | PAN 15 | 2 | 14,000 |
| | | 13. | PAN 3M-05 | 2 | 14,000 |
| | | 14. | PAN 53 | 2 | 14,000 |
| | | 15. | PAN 4M-19 | 2 | 14,000 |
| | | 16. | PHB 3253 | 2 | 14,000 |
| | | 17. | ETG M 601 | 2 | 14,000 |
| | | 18. | Kaspidi | 2 | 14,000 |
| | | 19. | Lubango | 2 | 14,000 |
| | | 20. | H 513 | 2 | 14,000 |
| | | 21. | DH 04 | 2 | 14,000 |
| | | 22. | H 625 | 2 | 14,000 |
| | | 23. | H 628 | 2 | 14,000 |
| | | 24. | H 614 | 2 | 14,000 |
| | | 25. | MAMSH 457 | 2 | 14,000 |
| | | 26. | WE4102 | 2 | 14,000 |
| | | 27. | MAMSH 458 | 2 | 14,000 |
| | | 28. | MERU VAH 517 | 2 | 14,000 |
| | | 29. | MERU VAH 519 | 2 | 14,000 |
| | | 30. | MERU HB 405 | 2 | 14,000 |
| | | 31. | MERU HB 513 | 2 | 14,000 |
| | | 32. | MERU HB 623 | 2 | 14,000 |
| | | 33. | WE 4114 | 2 | 14,000 |
| | | 34. | SC 303 | 2 | 14,000 |
| | | 35. | SC 403 | 2 | 14,000 |
| | | 36. | SC 419 | 2 | 14,000 |
| | | 37. | SC 513 | 2 | 14,000 |
| | | 38. | SC 555 | 2 | 14,000 |
| | | 39. | SC 657 | 2 | 14,000 |
| | | 40. | TZH 536 | 2 | 14,000 |
| | | 41. | TZH 538 | 2 | 14,000 |
| | | 42. | KH 500-43A | 2 | 14,000 |
| | | 43. | EAS401 | 2 | 14,000 |
| | | 44. | WH 509 | 2 | 14,000 |
| | | 45. | WH 605 | 2 | 14,000 |
| | | 46. | WH 403 | 2 | 14,000 |
| | | 47. | WH 505 | 2 | 14,000 |
| | | 48. | ZMS 606 | 2 | 14,000 |
| | | 49. | ZMS 405 | 2 | 14,000 |
| | | 50. | ZMS 402 | 2 | 14,000 |
| | Aina za Mbegu Chotara (Hybrid) zinazokomaa kwa muda mrefu | 1. | DK 777 | 2 | 14,500 |
| | | 2. | DKC 90-89 | 2 | 14,500 |
| | | 3. | PAN691 | 2 | 14,500 |
| | | 4. | SC 719 | 2 | 14,500 |
| | | 5. | ZMS 638 | 2 | 14,500 |

4. Vyombo vya Serikali vitahakikisha kuwa uuzaji wa mbegu zote za mahindi zilizothibitishwa ubora kwa mpango wa ruzuku unazingatia mwongozo utakaotolewa na Wizara ya Kilimo na bei elekezi zilizotajwa kwenye jedwali lililopo katika kipengele cha 3 hapo juu.

5. Ninapenda kusisitiza kuwa hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka maelelkezo ya Serikali. Maelekezo mengine ya kiutendaji yataendelea kutolewa na Serikali kwa kadri itakavyohitajika. Mawasiliano zaidi yanaweza kufanyika kupitia anuani ya barua pepe info@tosci.go.tz.

**IMETOLEWA NA:**
**Patrick Ngwediagi**
**MKURUGENZI MKUU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

TAASISI YA KUTHIBITI UBORA WA MBEGU TANZANIA

TOSCI

**TAARIFA KWA UMMA**

## ORODHA YA NYONGEZA YA AINA ZA MBEGU ZA MAHINDI KWENYE MFUMO WA RUZUKU

Zifuatazo ni aina za mbegu za nyongeza kwenye jedwali lililotolewa katika tangazo la utoaji wa ruzuku ya mbegu za mahindi zilizothibitishwa ubora la tarehe 02/09/2024.

| Kundi | | Na. | Aina ya mbegu | Uzito (Kilo) | Bei kikomo yenye ruzuku (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Aina za Mbegu zinazochavushwa huria (OPVs) | 1. | SITUKA M2 | 2 | 7,000 |
| II | Aina za Mbegu chotara (Hybrid) zinazokomaa mapema na muda wa kati | 1. | UHS 5350 | 2 | 14,000 |
| | | 2. | UH 6305 | 2 | 14,000 |
| | | 3. | UHS 401 | 2 | 14,000 |
| | | 4. | ZR8643 | 2 | 14,000 |
| | | 5. | P2848W | 2 | 14,000 |
| | | 6. | PAN 4M-11 | 2 | 14,000 |
| | | 7. | H 624 | 2 | 14,000 |
| | | 8. | H 6213 | 2 | 14,000 |
| | | 9. | KS H 519 | 2 | 14,000 |
| | | 10. | MERU HB 515 | 2 | 14,000 |
| | | 11. | ADV2308W | 2 | 14,000 |
| | | 12. | TZM 523 | 2 | 14,000 |
| | | 13. | EAS 5019 | 2 | 14,000 |
| | | 14. | ZMS 528 | 2 | 14,000 |
| | | 15. | ZMS 520 | 2 | 14,000 |
| III | Aina za Mbegu Chotara (Hybrid) zinazokomaa kwa muda mrefu | 1. | H6302 | 2 | 14,500 |
| | | 2. | ETG M601 | 2 | 14,500 |
| | | 3. | ZMS 720 | 2 | 14,500 |

**IMETOLEWA NA:**

Patrick Ngwediagi
**MKURUGENZI MKUU**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA: UPUNGUZAJI WA KIWAMGO CHA HEWA YA UKAA (KABONI): UJENZI WA MAUNGANISHO YA GRIDI NA MIFUMO YA BESS (INATANGAZWA TENA) KUMBUKUMBU NA.00000527**

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma ya Upunguzaji wa Kiwamgo cha hewa ya Ukaa (Kaboni): Ujenzi wa Maunganisho ya Gridi na mifumo ya BESS kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalosafirisha mafuta ghafi kuanzia eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka mashariki mwa pwani ya Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani katika Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Nchini Tanzania, bomba litapita katika mikoa nane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27, na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
**Maombi ya kuonesha nia yenye kumbukumbu na EOI ya REQ-00000527 yalitangazwa hapo awali tarehe 07 Mei 2024 yakiwa na mawanda yafuatayo:**

**U**handisi, **U**gavi, **U**jenzi na **U**zinduzi wa:

- Vituo vya kuunganisha gridi yenye 33kV na mifumo yake ya udhibiti na mifumo ya huduma za kijamii ikijumuisha transfoma ya 33kV/33kV na njia za 33kV kwa ajili ya uchepushaji.
- Mifumo ya BESS ya 33kV na mifumo yake ya udhibiti (ili kuleta utulivu wa nishati ya gridi na kufanya kazi ya Kubadilisha Umeme (kutoka matumizi ya nishati ya gridi hadi matumizi ya nishati ya nje ya gridi).
- Mifumo yote ya udhibiti wa umeme inayojulikana kama Mfumo wa Usimamizi wa Umeme na huweka kipaumbele cha usambazaji wa umeme kwa EACOP.
- Nyaya zote zinazohusiana na utoaji wa nishati na udhibiti.
- Kazi zote zinazohusiana na ujenzi( barabara za kuingilia, misingi, mitaro nk)
- Mifumo yote inayohusiana na mawasiliano ya simu na ulinzi (CCTV, Uzio, get ink)

**Maombi ya kuonesha nia kumbukumbu na: EOI ya REQ-00000527 yamefanyiwa maboresho na kutangazwa upya katika mawanda yafuatayo:**

Ujenzi wa:

- Vituo vya kuunganisha gridi yenye 33kV na mifumo yake ya udhibiti na huduma za kikamii ikijumuisha transfoma ya 33kV/33kV na njia za 33kV kwa ajili ya uchepushaji.
- Mifumo ya BESS ya 33kV na mifumo yake ya udhibiti (ili kuleta utulivu wa nishati ya gridi na kufanya kazi ya Kubadilisha Umeme (kutoka matumizi ya nishati ya gridi hadi matumizi ya nishati ya nje ya gridi).
- Mifumo yote ya udhibiti wa umeme inayojulikana kama Mfumo wa Usimamizi wa Umeme na kuweka kipaumbele cha usambazaji wa umeme kwa EACOP.
- Nyaya zote zinazohusiana na utoaji wa nishati na udhibiti.
- Kazi zote zinazohusiana na ujenzi( barabara za kuingilia, misingi, mitaro nk).
- Mifumo yote inayohusiana na mawasiliano ya Habari na ulinzi ( CCTV, Uzio, get ink).

Kwa ajili ya kituo cha pampu namba 3 kilichopo Bukoba, kituo cha pampu namba 4 cha Shinyanga, kituo cha pampu namba 5 cha Shinyanga, kituo cha pampu namba 6 cha Singida na kituo cha kuhifadhi mafuta cha Baharini kilichopo Tanga.

Mifumo ya BESS na vifaa vyote vitatolewa kwa Mkandarasi aliyechaguliwa bila malipo na EACOP na vitatandazwa na Mkandarasi wa Ujenzi aliyechaguliwa.

**VIGEZO MUHIMU:**
**Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:**

- Maelezo mafupi ya uzoefu, utaalamu, na uwezo wa kutoa huduma katika wigo husika.
- Maelezo ya miradi au shughuli zinazofanana zilizokwishafanywa zinazotoa uthibitisho wa timu iliyopo yenye weledi, uelewa wa maeneo ya bomba, na rekodi ya uzoefu ulioorodheshwa hapo juu.
- Leseni ya biashara.
- Cheti cha usajili na Uthibitisho wa usajili wa BRELA wa havi karibuni (ambatanisha nakala).
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Sera YA Haki za Binandamu.
- Ubobezi katika Uhandisi na Ugavi wa mifumo ya kutunza wa Umeme wa Betri.
- Pale inapohitajika, uthibitisho wa usajili wa bodi za kitaaluma, kwa mfano Bodi ya usajili ya Wahandisi au Bodi ya Usajili ya Wakandarasi.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu zinapaswa kuonesha nia zao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **04 Oktoba 2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000527– Upunguzaji wa Kiwamgo cha hewa ya Ukaa (Kaboni): Ujenzi wa Maunganisho ya Gridi na mifumo ya BESS.**
**Makampuni na mashirika ambayo mwanzo yalionyesha nia katika EOI iliyotolewa tarehe 07 Mei 2024 yanahimizwa kutuma maombi upya ya kulingana na mawanda yaliyoboreshwa.**
Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.
**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.**

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na tangazo hili la kuonesha nia na kufanya tathmini kwa kuzingatia vigezo vya ndani ili kubaini kampuni ambazo zitakazojumuishwa kwenye orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD inaheshimu haki katika kufanya maamuzi ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

# ACT yatua THBUB wananchi kufanyiwa ukatili

**Na Grace Mwakalinga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimepeleka madai ya uvunjifu wa haki za binadamu kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Wizara ya Katiba na Sheria na nakala kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukatili unaodaiwa kufanyiwa wananchi wa vijiji 11 vya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora.

Madai hayo ni mauaji ya watu 12 wa vijiji 11 vya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, kuuawa na wanaodaiwa ni Askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS), kwa sababu ya mgogoro wa ardhi katika Pori la Akiba la Igombe.

Aidha, kaya kati ya 7,000 hadi 8,000, ziliondolewa kwenye ardhi yao na kuachwa bila makazi, wengine walinyang'anywa mali zao kama vile mifugo, mazao, vipigo, kubambikiziwa kesi na kutozwa faini.

Naibu Katibu wa Idara ya Haki za Binadamu na Vyombo vya Uwakilishi wa Wananchi ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria wa chama hicho, Mbarala Maharagande jana alisema, wamefikia uamuzi huo baada ya kuona hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi ya waliohusika na uvunjifu wa haki za binadamu.

"Tumechukua hatua juu ya yote yaliyofanyika kwenye Vijiji vya Usinge, Luganjo, Wachawaseme, Igagala, Kombe, Tuombe Mungu, na Limbu la Siasa, watu kuuawa, mali zao kuporwa na wengine kubakwa, ACT-Wazalendo tunaamini suala hili lipo kwenye mikono salama na hatua stahiki zitachukuliwa dhidi ya wale wote waliohusika na uvunjifu wa haki za binadamu," alisema Maharagande.

Alisema wapo tayari kutoa ushirikiano na ushahidi kuhusu madai yao waliyoyapeleka THBUB kwa sababu wamefanya utafiti na wana vielelezo vya kutosha.

Akieleza historia ya madai hayo, Maharagande alisema umetokana na serikali kupitia TAWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na uongozi wa Wilaya ya Kaliua kuchukua eneo la hifadhi ya ardhi ya vijiji 11 na kubadilisha kuwa Pori la Akiba la Igombe bila ridhaa yao.

Aliongeza kuwa, mwaka 2007 vijiji 11 vilikubaliana kutenga sehemu za ardhi yao yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,800 kwa ajili ya kuanzisha jumuiya ya hifadhi ya wanyama pori iliyojulikana kwa jina la Igombe na Sagara Wildlife Management Area (ISAWINA).

Kutokana na uhaba wa ardhi na ongezeko la watu kati ya mwaka 2016 na 2021, wananchi walifikia makubaliano ya kupunguza ukubwa wa eneo lao la hifadhi hadi kilomita za mraba 1,300 na kuacha 500 kwa matumizi ya ardhi ya vijiji.

Aidha, alifafanua kuwa serikali ilichukua kilomita 1300 na kuanzisha Pori la Akiba la Igombe na kuacha kilomita 500 kwa Tangazo la Serikali (GN) namba 455 la mwaka 2021 hata hivyo, kilomita zilizoachwa na wananchi zilichukuliwa na uongozi wa ISAWINA.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha akiwa katika moja ya nyumba za ibada mkoani humo, alikanusha kuwapo kwa mauaji ya wananchi katika vijiji hivyo, nyumba kuchomwa na watu kubakwa pamoja na kulawitiwa.

Alisema wanahitaji Maharagande ambaye alizungumza kupitia vyombo vya habari kutoa ushahidi wa kumpata mtu aliyehusika kufanya matukio hayo ya uhalifu badala ya kuendelea kuzua taharuki na kuibua hofu kwa jamii.

Haya si mambo ya kuyaacha huyu mtu tunataka atuoneshe hawa waliouawa wapi, kwenye familia zipi na walizikwa wapi, waliobakwa na kulawitiwa na nani, nimewaambia mawakili, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, atuoneshe matukio hayo, hatuwezi kuyafumbia macho, afikishwe kwenye vyombo vya sheria," alisema Chacha.

Alisema serikali inamtaka Maharagenda kuthibitisha tuhuma hizo alizozielekeza kwa askari wa TAWA na TFS.

# Wahamasishwa matumizi ya mbolea ruzuku kwa usahihi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, amesema licha ya wilaya hiyo kuwa kinara wa matumizi ya mbolea ya ruzuku kulinganisha na nyingine, kuna haja kwa wataalamu wa kilimo kuhamasisha wakulima kuitumia kwa usahihi, ili kuleta matokeo mazuri zaidi.

Akizungumza jana wakati wa mkutano na wakulima wa mkoani Morogoro uliofanyika wilayani humo, Shaka aliwakumbusha wakulima kusajiliwa katika mfumo wa kidigitali wa mbolea ya ruzuku.

Aliwataka wafanye hivyo, ili kuendelea kunufaika na fursa hiyo inayotolewa na serikali kwa ajili ya wakulima wote nchini.

Kadhalika aliwasisitiza wakulima kuzingatia maelekezo ya wataalamu kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya mbolea, badala ya kusikiliza kauli za wakulima zinazopotosha maana halisi ya mbolea katika mmea. "Serikali imewekeza nguvu kubwa ya hali na mali katika sekta ya kilimo ikiwamo, kuajiri maofisa ugani wa kutosha, kuweka ruzuku katika mbolea, vitendea kazi kwa maofisa ugani. "Kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo. Jukumu letu wakulima ni kuhakikisha, tunazitumia fursa hizo vizuri kwa ajili ya matokeo mazuri shambani," alisema Shaka.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Elizabeth Bolle, alisema takwimu za matumizi ya mbolea zinaonesha, wilaya hiyo katika msimu wa 2023/24, imetumia jumla ya tani 4,554.8 ikilinganishwa na tani 2,652.1, zilizotumika na wakulima wa wilaya hiyo katika msimu wa 2022/23, sawa na ongezeko la tani 1,902.7.

Bolle alisema kuwa jumla ya wakulima 23,852, wamesajiliwa katika mfumo wa kidijitali, ikiwa ni zaidi ya lengo la kusajili wakulima 20,000 wa Wilaya ya Kilosa.

"Pamoja na takwimu hizo, Mamlaka inaamini kuwa bado kuna wakulima ambao hawajajisajili, hivyo ninaomba nitumie nafasi hii kuwasihi wakulima wa wilaya hii na Mkoa wa Morogoro, ambao hawajasajiliwa, waende kujisajili katika mfumo wa kidijitali kupitia Ofisi za Watendaji wa Vijiji na Mitaa", alisema Bolle. Kwa mujibu wa Bolle, pamoja na wakulima kunufaika na mpango wa mbolea ya ruzuku, kanzi data ya usajili wa wakulima itaisaidia serikali kuweka mipango sahihi ya kuendeleza Slsekta ya kilimo na kuwawezesha wakulima kupata huduma nyingine kama vile huduma za ugani, taarifa za masoko ya mazao, huduma za kifedha na huduma nyinginezo.

Mkoa wa Morogoro unajulikana kwa kilimo cha mazao mbalimbali ikiwamo mahindi, mpunga, miwa, viungo, mbogamboga na matunda, hivyo mkutano huo unaolenga kutoa hamasa ya matumizi sahihi ya mbolea na kuhamasisha usajili kupitia kampeni ya Kilimo ni mbolea.



# Mradi kuendeleza kahawa waleta matokeo chanya

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MRADI wa kuendeleza zao la kahawa unaofadhiliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Afrika ya US African Development Foundation (USADF), umeanza kuonesha matokeo chanya baada ya wakulima 850 wa ukanda wa juu wa Lukani na Losaa wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, kuhamasisha zaidi ushiriki wa vijana.

Akizungumzia matokeo hayo jana, Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Kahawa cha Lukani/Losaa Amcos Limited, Ebenetho Munuo, alisema mradi huo umeongeza uzalishaji kwa kuhamasisha wakulima wapya, upanuzi wa mashamba na uhamasishaji wanawake kushiriki kwenye uongozi wa chama.

USADF inaratibiwa na Serikali ya Watu wa Marekani, inalenga zaidi kuamsha ari ya uzalishaji wa zao hilo na kujenga uwezo kwa wakulima wa kahawa, kurejesha imani ya kustawisha tena zao hilo lenye tija kubwa kiuchumi.

"Masharti makubwa ya ruzuku hii ya Sh. milioni 250 zilizotolewa na USADF, ni kuelekeza fedha za mradi kwenye ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji na uchakataji wa kahawa. lingine ni kuboresha miundombinu ya umwagiliaji.

**"Masharti makubwa ya ruzuku hii ya Sh. milioni 250 zilizotolewa na USADF, ni kuelekeza fedha za mradi kwenye ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji na uchakataji wa kahawa. lingine ni kuboresha**

Zaidi aliongeza: "Uhifadhi wa mazingira, kuimarisha mifumo na kutoa maarifa na taarifa muhimu kuhusu uzalishaji bora na wenye tija. Kuweka mfumo wa kielektroniki wa kuweka kumbukumbu za fedha na kahawa pamoja na kurahisisha mfumo wa malipo kwa mkulima, hususani kuwezesha matumizi ya mfumo maalum wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania (MUVU).

Kabla ya kupatikana kwa ruzuku hiyo, Lukani/Losaa Amcos Limited ilikuwa ikikabiliwa na changamoto ya kutokuwapo kwa usafiri wa ajili ya kusafirisha kahawa za maganda kutoka kwa wakulima kupeleka kiwandani na uwezo mdogo wa kugharamia mafunzo ya mbinu bora za kilimo cha kahawa.

Changamoto nyingine ni kukosekana kwa mfumo mzuri wa kisasa na nafuu wa kuwezesha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima na hitaji la kuongeza uwezo wa uchakataji wa kahawa kwa mategemeo ya ongezeko la kahawa.

Hata hivyo, chama hicho kinacho fursa za masoko ya moja kwa moja ya kuuza kahawa Japan, Marekani, Australia na China zilizoonesha nia ya kununua kahawa yao kwa msimu ujao wa 2025/2026. Bei ya mkulima imepanda kutoka Sh.4,000 hadi 6,500 kwa kahawa inayomenywa majumbani (HP), huku bei ya kahawa inayopitia CPU ikiongezeka kutoka Sh. 5,000 hadi 8,000 kwa kilogramu moja.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Dk. Juma Mhina, akipanda mti kwa ajili ya kutunza mazingira, wakati wa utambulisho wa kampeni ya "Mtoto wa Leo, Samia wa Kesho", katika Shule ya Msingi Kazita, Kata ya Misalai, wilayani humo hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Madiwani walia fidia ndogo inayotolewa na TAWA

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wamelalamikia fidia ndogo wanayopata kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA), pindi wanapopata majanga yanayosababishwa na wanyamapori.

Madiwani hao wamelalamikia fidia ndogo au kutopata kabisa pindi wanyamapori wakijeruhi mtu au wanapokula mazao mashambani, wakati walipokuwa jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Simanjiro.

Diwani wa Kata ya Naisinyai, Taiko Kurian, alisema baadhi ya wananchi wa eneo lake walijeruhiwa na tembo ila hawakulipwa japokuwa walifuatilia na kutoa taarifa.

"Zaidi ya hayo, hata hiyo fidia inayosemwa itatolewa pindi mtu akipata majanga ni ndogo, kwani wanyamapori wakishambulia mtu au wakila mazao, fidia inayotolewa ni kidogo mno," alisema Taiko.

Diwani wa Kata ya Msitu wa Tembo, Kaleiya Mollel, alisema matukio ya mazao kuliwa na tembo au watu kujeruhiwa yametokea mara nyingi ila hawapati fidia wala kifuta machozi.

Aidha, Diwani wa Kata ya Mirerani, Salome Mnyawi, alisema jamii inalalamikia changamoto hizo. Hivyo, TAWA wachukue hatua kwa kurekebisha viwango vyao.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jacob Kimeso, alisema kuna baadhi ya wanyama wanaua watu, ila hawapo kwenye orodha ya fidia, hilo linapaswa kuangaliwa.

Aliwataja wanyama ambao hawako kwenye orodha ya malipo ni nyoka au kicheche.

Kimeso alisema kwenye kata yake kuna watu wawili walifariki dunia kwa kung'atwa na kicheche ambaye ana sumu na hakuna fidia yoyote waliyopata.

Mkuu wa TAWA, Idara ya Ujirani Mwema ya Ikolojia ya Handeni/Kitwai, Ambokile Mwakyusa, alisema kumepitishwa sheria mpya na kanuni mpya za fidia pindi wanyamapori wakijeruhi, kuua au kuharibu mazao.

Mwakyusa alisema viwango hivyo vimebadilika ambapo mtu akiuawa na mnyama inatolewa kifuta machozi cha Sh.milioni 2, awali ilikuwa Sh. milioni moja.

Alisema mtu akijeruhiwa na kupata ulemavu wa kudumu, alikuwa anapata Sh. 500,000 na sasa ni Sh. milioni moja na kama ni ulemavu wa kupona anapata Sh.500,000.

Mwakyusa alisema kwa upande wa mazao wanatoa fidia kwa ekari moja Sh.375,000 pindi wanyamapori wakifanya uharibifu kwenye shamba.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Baraka Kanungaa, alimuagiza kiongozi huyo wa TAWA kufikisha mapungufu yaliyoelezwa na madiwani hao ili yaweze kufanyiwa kazi.

# Watu 34,488 watibiwa bure magonjwa ya macho

**Na Thobias Mwanakatwe,** KOROGWE

WAGONGWA wa macho 34,488 wamepatiwa huduma za matibabu bure kupitia ufadhili wa Taasisi ya Mo Dewji Foundation iliyotolewa katika mikoa sita nchini.

Kati ya wagonjwa hao, 2,327 waliokuwa wakisumbuliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo mtoto wa jicho, uvimbe wa nyama kuota kwenye jicho walifanyiwa upasuaji.

Mratibu wa Miradi ya Taasisi ya Mo Dewji Foundation, Amina Ramadhan, alisema hayo juzi wakati wa utoaji huduma za matibabu ya magonjwa ya macho kwa siku tatu yakiyokuwa yakifanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga.

Alisema wagonjwa hao wamepewa matibabu hayo katika kambi zilizofanyika kwa muda wa miezi nane katika mikoa ya Singida, Lindi, Dodoma, Mtwara, Morogoro na Tanga.

Alisema katika kipindi hicho pia wagonjwa wa macho 14,509 walipewa miwani bure na wengine 21,760 walipewa dawa za macho.

Alisema: "Kambi za matibabu ya macho kwa Mkoa wa Singida zilifanyika Manispaa ya Singida, Mkoa wa Lindi katika Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Dodoma ilifanyika Wilaya ya Kondoa, Mtwara Masasi, Morogoro ilifanyika katika Wilaya ya Ifarakara wakati kwa Mkoa wa Tanga huduma zilifanyika katika Wilaya ya Muheza, Manispaa ya Tanga na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe".

Alisema kuwa, Taasisi ya Mo Dewji Foundation imejiwekea malengo katika kipindi cha mwaka mmoja iweze kuwafikia wananchi 50,000 kuwapatia bure huduma za matibabu ya macho.

Daktari wa Macho, Salim Mohamed, alisema idadi kubwa ya wagonjwa katika kambi walizofanya inatokana na wananchi kuwa mbali na huduma za kibingwa za macho zinakotolewa.

Alisema tatizo la mtoto wa jicho ambalo wagonjwa wengi wamegundulika kuwa nalo linatokana na umri mkubwa, kuumia na kuwa na presha au ugonjwa wa kisukari.

Hadi mchakato wa kutoa matibabu unahitimishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe wagonjwa 4,228 walihudumiwa, 376 walifanyiwa upasuaji, 1,999 walipewa miwani ya macho na 2,790 walipewa dawa.





# TRA yawabana makandarasi ulipaji kodi kwa wakati

**Na Benny Kingson,** TABORA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Tabora imewataka makandarasi wanaotekeleza miradi mkoani humo kuhakikisha wanalipa kodi kwa wakati ili kusaidia utekelezaji wa malengo ya mamlaka hiyo ya kukusanya Sh. trilioni 30.4 mwaka 2023/24.

Wito huo umetolewa juzi na Meneja wa TRA Mkoa wa Tabora, Fedrick Kanyilili wakati akifungua mafunzo ya elimu ya mabadiliko ya sheria mpya ya ulipaji kodi kwa makandarasi.

Kanyilili alisema ulipaji kodi ni muhimu kwa maendeleo ya jamii pia kuimarisha uchumi wao na wa umma, hivyo aliwashauri walipe kodi kwa wakati pia kuepuka usumbufu na kupigwa faini.

"Leteni 'retuns' zenu kwa wakati na muwe wazalendo wa kweli kwa kulipa kodi kwa wakati bila kushurutishwa pia kuendelea kujenga heshima yenu kwa wadau mnao wahudumia pia serikali kuwapa tenda za kazi," alisema.

Kadhalika, aliwataka kuhakikisha wanatumia risiti za kieletroniki za EFD pindi watoapo huduma au kupata huduma mahali popote na kucha kabisa kutumia risiti za mkono ambazo hazitambuliki kisheria.

"Tuepuke kuchelewa kulipa kodi ili kutopigwa faini ambazo zinaumiza. TRA ipo kwa ajili ya kuwahudumia wadau wote na hatupo kwa ajili ya kuwapiga faini ambako ni kuruhusu kirusi kingie kwenye kazi zetu na kuleta chuki miongono mwetu" alisema Kanyilili.

Mwenyekiti wa makandarasi Mkoa wa Tabora, Frank Mgonja alisema kuna haja kwa mamlaka hiyo kushirikiana na uongozi wa makandarasi mkoani humo kuwatambua wanachama walio hai, badala ya kuwa na orodha ndefu isiyokuwa na uhalisia.

# Nyani wavamia makazi, hofu maambukizi mpox yatanda

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMULO

WAKATI serikali ikiendelea kuchukua tahadhali za ugonjwa wa mpox, baadhi ya wakazi wa maeneo ya mpakani wilayani Biharamulo mkoani Kagera wameiomba serikali kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti ugonjwa huo usiingie nchini.

Wametoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakidai kuishi kwa hofu ya kuambukizwa ugonjwa huo, kutokana na ongezeko la nyani wanaodaiwa kutoroka katika Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato, kisha kujeruhi watu, kula mifugo, mazao na kutishia usalama wa wananchi. Diwani wa Kata ya Nyarubungo, Petro Kizuluja, alisema wanyama hao wamegeuka kuwa tishio la uhai wa jamii kutokana na tukio la hivi karibuni kwenye Kijiji cha Lusabya, ambapo mtoto mdogo (jina linahifadhiwa) aliibwa na nyani kabla ya kunusuliwa na wananchi.

**"Mtoto huyo alichukuliwa wakati mama yake akiendelea na shughuli za shambani lakini aliokolewa na wananchi na kukutwa amejeruhiwa maeneo ya uso na masikio,"**

"Mtoto huyo alichukuliwa wakati mama yake akiendelea na shughuli za shambani lakini aliokolewa na wananchi na kukutwa amejeruhiwa maeneo ya uso na masikio," alisema Kizuluja.

Diwani wa Kata ya Ruziba, Athanas Sumbuso, alisema wanyama hao mbali na kutishia uhai na afya ya watu huenda wakasababisha njaa kutokana na uharibifu wa mazao shambani pamoja na mifugo inayoshambuliwa na kuliwa.

"Kitendo cha nyani kuendelea kuwapo kwenye makazi ya watu ni tishio kubwa zaidi la ugonjwa wa mpox kwa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hiyo, kwa kuwa wanaweza kuwaambukiza wananchi hao baada ya kuwajeruhi au kwa kushiriki chakula kilicho chafuliwa na wanyama hao," alisema.

Ofisa Maliasili wa Halmashauri hiyo, Thomas Mahenge licha ya kukiri kuwapo kwa hatari hiyo, alisema jitihada za kuwaondoa wanyama hao zinataratibu zake ikiwamo kuwaomba Mamlaka ya Utafiti wa Wanyama Pori Nchini (TAWIRI) kuchunguza mazingira sahihi ya kuwahamishia.

Kadhalika, alisema suala hilo huenda likachukua muda mrefu kutokana na tishio la uwapo wa ugonjwa wa mpox, licha ya awali kufanyika baadhi ya jitihada za kuwazuia kuharibu mazao ya wananchi.

"Hata hivyo, uchunguzi wetu umebaini kuwa nyani waliopo eneo hilo hawana uhusiano na wengine waliopo porini, kwa maana huo ni ukoo tofauti, ndiyo maana wao wanapatikana kwenye eneo lenye mawe tofauti na wengine walioko porini" alisema Mahenge.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Leo Rushahu, alimtaka Ofisa Maliasili wa Wilaya kufanya mawasiliano ya dharura na TANAPA ili kutafuta njia mbadala ya kuwaondoa wanyama hao.



Aliyekuwa mkazi wa Kijiji cha Nyatwali, wilayani Bunda, mkoani Mara, Deo Mgengeli, akiihudumia mifugo yake katika makazi mapya ya Nyanguge, wilayani Magu, mkoani Mwanza juzi, baada ya kuhama kijijini hapo, ambapo serikali inajiandaa kuwalipa fidia wakazi wa kijiji hicho, ili kupisha eneo hilo, kwa ajili ya Hifadhi ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asilimia 80 wanaopiga simu M-Mama wanatukana

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI 43 kati ya 50 wanaopiga simu ya dharura ya kuomba huduma ya usafiri wa wajawazito na watoto (M-Mama) kwa siku, mkoani Shinyanga wamedaiwa kutokuwa na uhitaji wa huduma husika, bali huwatukana wahudumu wa huduma hiyo.

Malalamiko hayo yametolewa jana na Muuguzi Kiongozi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga kitengo cha M-Mama, Joyce Magaya, wakati akizungumza na Nipashe hospitalini hapo.

Alisema huduma hiyo inayotolewa kupitia simu ya bure 115 ni kwa ajili ya wajawazito na watoto kuomba usafiri wa dharura ili wawahishwe kwenye huduma za afya na kupata matibabu haraka, lakini baadhi ya watu hutumia huduma hiyo vibaya, kwa kupiga simu na kuanza kutukana matusi au kusikilizisha mziki.

"Tusaidieni kuelimisha wananchi waache tabia ya kupiga simu na kuanza kutukana matusi, simu inapigwa ukipokea unasikia tusi we pumbavu au unasikilizishiwa muziki hii siyo sawa," alisema Joyce. Alisema kwa siku moja anaweza kupokea simu 50 zenye matusi lakini za watu ambao wanaohitaji huduma hiyo ni simu sita hadi saba, hivyo aliwasihi wananchi wasiitumie namba hiyo ya dharura vibaya, sababu inasababisha wajawazito kukosa huduma kwa wakati kutokana na simu kutumika isivyo sahihi.

Aidha, alisema huduma hiyo ya M-Mama imesaidia kwa kiasi kikubwa katika Mkoa wa Shinyanga kwa kupunguza vifo vya wajawazito vitokanavyo na kuchelewa kufika kwenye huduma za afya, sababu ikipigwa simu ya dharura 115 usafiri wake hupatikana haraka na mjamzito anawahishwa hospitali. Baadhi ya kina mama wa Shinyanga akiwamo Ashura Maliki, waliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria watu hao ili kusaidia huduma hiyo kuendelea kutolewa kwa ufanisi.

Alisema: "Watafutwe hata wawili tu watolewe mfano ili kukokomesha vitendo hivyo, kwani huduma hiyo ni muhimu katika kuokoa maisha ya mjamzito na mtoto".


# ama

**ALHAMISI SEPTEMBA 5, 2024** AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Ujue ukweli kuhusu chupa za plastiki za maji hazileti saratani**



**MAAJABU KISUKARI CHA MBUNGE... Dk. Malima aligundua kwa simu, Janabi akaendeleza safarini**

Ukurasa 13

## TAKA ZINAPOGEUZWA MALIGHAFI...

# Waingia kazini kutekeleza mbadala wa Rais, kuacha mkaa uliozoeleka

• Darasa laanza nyumbani, kisha wajasiriamali wadogo

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI serikali ikiendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ikilenga asilimia 80 ya Watanzania watumie nishati hiyo mpya kama Rais alivyoagiza, wadau katika kikundi cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Dar es Salaam wameanza mchakamchaka kuitikia kwa namna yao.

Hilo wanalifanya wakiwafundisha majumbani wanawake wajasiriamali wenye ulemavu, namna ya kutengeneza mkaa mbadala wakitumia taka mbalimbali, zikiwamo zinazoweza kuloanishwa na maji.

Kurejea mzizi wa utekelezaji huo, mnamo Oktoba 5 mwaka jana, aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, akafafanua kuwa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameibeba kwa dhati ajenda ya matumizi ya nishati mbadala kutokana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Katika kauli yake hiyo mkoani Ruvuma, sanjari na ugawaji majiko, mitungi ya gesi iliyotolewa na serikali, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Naibu Waziri akafafanua:

"Ninyi nyote mnafahamu ajenda ya Mheshimiwa Rais kuhusiana na umuhimu wa nishati mbadala. Tunafahamu changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na changamoto za mazingira kwa ujumla.

'Hii ni ajenda ambayo Rais ameibeba kwa dhati kabisa, kuhakikisha tunaanza mchakato wa kuelimisha Watanzania, ili kuondokana na nishati ambazo sio rafiki kwa mazingira na kutumia zilizo rafiki kwa mazingira,".



Kinamama wakionyesha kwa vitendo, namna ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutwanga malighafi kwenye kinu. Hiyo ni baada ya kupata mafunzo, kutoka Asasi ya Sauti ya Jamii Kipunguni, Ukonga Dar es Salaam. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

Tamko hilo la Naibu Waziri Kapinga, ni mwendelezo wa kilichojiri mwaka mmoja kabla, Novemba 2022, Rais Dk. Samia, aliposhiriki 'mjadala wa kitaifa kutafuta suluhu ya nishati safi ya kupikia,' alioyotafsiri kuwa "hatua ya kwanza kuelekea suluhisho ni Watanzania wenyewe kubadilisha mtazamo wao."

Taarifa zilizotolewa katika mjadala huo, ni kwamba Watanzania wanatumia nishati safi walikuwa asilimia tano pekee, waliobaki wakizama katika kuni na mkaa, hali iliyotajwa chanzo cha vifo takribani 33,000 kila mwaka nchini.

Akizungumza wakati akizindua mjadala huo wa kitaifa wa siku mbili, Rais Dk. Samia, ambaye ni mdau wa kutetea mazingira kitaifa, akanena hatua ya kwanza kupambana na matumizi ya kuni na mkaa, ni kwa Watanzania wenyewe kubadili mitazamo.

Rais Samia akafafanua kwamba matumizi ya kuni na mkaa ni suala mtambuka nchini; chanzo cha ukame unaosababisha uhaba wa maji, magonjwa na kusababisha unyanyasaji kijinsia katika jamii.

**INAVYOTEKELEZWA KIPUNGUNI**

Mkurugenzi wa kikundi, Seleman, Bishagazi, anasema lengo lao ni kuwafundisha wanawake hao kutengeneza mkaa huo ili iwapunguzie ukali wa maisha katika bajeti ya mkaa uliozoeleka.

Bishangazi anasema, wameanza na wanawake wa maeneo jirani ya Kivule na Majohe wilayani Ilala, wakilenga kufikishia elimu kwa kaya zaidi ya 200, zihamie katika mkaa mbadala.

Anafafanua; "Pia, wapo wanawake na wasichana wanaotumia zaidi ya saa sita kutafuta nishati ya kupikia. Kwa hiyo, tukiwafundisha kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumia taka zinazotokana katika maeneo yao, ukataji hovyo wa miti na uchomaji utapungua sana."

Hadi sasa, asilimia kubwa ya Watanzania wanategemea kilimo cha mvua au maji na kadri wanavyoendelea kukata miti, uwezekano wa kupata maji ya kutosha unabaki mdogo, mkombozi dhidi ya magumu hayo ni kutumia nishati mbadala na rafiki kwa mazingira, unaookoa mengi.

"Tunawafundisha teknolojia hii waione kwamba ni fursa, lakini wakati huohuo tunalinda mazingira na kuokoa misitu yetu kwa faida ya vizazi na vizazi na kuepusha magonjwa yanayotokana na matumizi ya mkaa ule."

Anasema kwamba, mafunzo ya kutengeneza nishati hiyo ya mkaa mbadala wamepewa na Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), ikiwa ji matokeo ya teknolojia mpya inayokinzana na ukataji miti hololela.

**WALENGA NA YAO**

Dorice Alfred ni mjasiriamali kutoka Kata ya Kivule, wilayani Ilala, anaeleza alivyonufaika katika ujasiriamali wake wa kupika uji na vitafunwa, mafunzo yamemsaidia pia kutunza fedha, tangu ajifunze kutengeneza mkaa unaotokana na taka, umeachana na mkaa wa miti.

"Mwanzoni nilikuwa natumia Sh.60,000 kwa mwezi kwa ajili ya kununulia mkaa wa kawaida, kila siku nilikuwa nanunua wa Sh.2000, lakini tangu nimejifunza na kuanza kutengeneza mwenyewe nimeokoa kiasi hicho cha fedha," anasema Dorice.

Anasema amejifunza kutengeneza mkaa wa aina mbili; wa taka zitokanazo na boksi, karatasi na mabaki ya baadhi ya vyakula.

Mjasiriamali Seya Khasad, anasema hakufahamu kama taka hizo ni fursa za kupatamkaa mbadala, akijieleza kuwa: "Mimi ni mama mjane na nyumbani ninaishi na familia kubwa wakiwamo wajukuu.

"Nilikuwa nateseka sana, un-

**Inaendelea Uk. 12**

AFYA

# Ujue ukweli unaohusu chupa za plastiki za maji hazileti saratani

Na Flora Wingia




CHUPA za plastiki kutumika kama kifungashio cha maji ya kunywa kwa matumizi ya binadamu, zimekuwa zikijadiliwa sehemu mbalimbali duniani, kuwa visababishi vya saratani.

"Hata hivyo, taarifa zilizopo kisayansi na kitafiti katika ukweli kuhusu matumizi ya plastiki kwa kufungashia vyakula na saratani, bado utafiti unaendelea," mtaalamu anasema.

Mshauri na Mtaalamu wa Afya ya Jamii, Dk. Ali Mzige, alipohojiwa hivi karibuni, alifafanuzi na kutoa ushauri kwamba ni vema watu wakafuata maagizo jinsi ya kuhifadhi, kupasha na kupika chakula wanapotumia vyombo vya plastiki.

Anasema, vyombo hivyo vinaweza kutumika tena, kwa kubadilishwa endapo vimeharibika au vina matobo.

Dk. Mzige anataja baadhi ya hoja anazozipinga ni matumizi ya plastiki na uhusiano wa saratani: Kwamba maji yanapogandishwa kwenye chupa za plastiki yanaweza kuleta saratani, au kutumia kila mara plastiki nako kunasababisha ugonjwa huo.

Pia, inatajwa chupa za maji za plastiki zinapowekwa juani au kwenye gari na kupata joto, kemikali za plastiki zinapovuja kwenye vifungashio vya vyakula vinaweza kusababisha saratani.

Vilevile, kunatajwa kusababisha saratani pale unapotumia 'microwave' kwa kupasha chakula wakati imefunikwa na plastiki, na vifungashio vya chakula vyenye kemikali ya 'dioxin'.

**UKWELI WAKE**

Dk. Mzige anasema, "ukweli wa mambo ni kwamba, chupa za maji za plastiki hutengenezwa kwa kutumia 'Polyethelene terephthalate (PET)', kemikali ijulikanayo kama DEHA zimesingiziwa kuwa zinaweza kuleta saratani. Katika utaalamu wa kemia, uhai na maabara, kemikali hizo hazipo katika kundi la kusababisha saratani."

Anasema, maji yapogandishwa kwenye chupa za plastki, hakuna uwezekano wa kemikali kutoka kwenye chupa ya plastiki.

Chupa za plastiki za maji zinaweza kutumika tena endapo zitaoshwa katika maji yenye vuguvugu na kutumia sabuni ya maji, ili atakayeitumia tena asipate maambukizi ya bakteria wala protozoa kama amoeba.

Chupa ya plastiki inapoharibika au ikionyesha kuchoka, ni vema ikabadilishwa. Kwa wanaotumia vifaa vya plastiki wanashauriwa watumie vifaa vinavyoweza kutumika kwenye 'microwave; joto lake kwenye gari haliwezi kutoa kemikali kwenye chupa za plastiki.

Akifafanua, anasema plastiki zinazotumika kufungia na kuhifadhi vyakula hutumia aina ya plastiki 'polyvinyl chloride' (PVC) kati ya kemikali iliyopo kwenye PVC, kemikali ya DEHA huifanya plastiki iwe laini.

Inapovuja huweza kuingia kwenye vyakula vyenye mafuta kama nyama, jibini mchakato huo huenda ukaleta madhara endapo 'microwave' itatumika kupasha vyakula kwenye hiyo plastiki.

**ANGALIZO LAKE**

Hakuna uthibitisho kuwa 'DEHA' inaweza kuleta saratani. Kiwango cha hizo kemikali za plastki hakijapita kiwango kilichopatikana kwenye wanyama waliofanyiwa utafiti kwenye maabara.

Anasema wanasayansi na watafiti wanashauri, binadamu achukue tahadhari, ambayo Dk. Mzige anashauri watu kutumia chombo cha plastiki kilichokubalika kutumika chenye maandishi 'suitable for microwave', yaani kinaweza kutumika kwenye 'microwave.'

Na kwamba vifungashio vya maziwa ya mtindi na 'ice cream' haviwezi kutumika kwenye 'microwave'. Kopo za plastiki zilivyohifadhi vipodozi anataja hazifai kuhifadhia chakula, au kugandishia maziwa.

Kuna aina ya plastiki ijulikanayo kwa jina 'Bisphenol A' (BPA). Plastiki hiyo ni nyeupe, inavumilia joto na haipasuki kirahisi, ndizo zinatumiwa kutengeneza chupa za maji, chupa za maziwa.

Aina hiyo ya plastiki hutumika kufungashia vyakula na vifuniko vya vyakula vya makopo.

Kemikali hiyo 'BPA' huenda ikaathiri mfumo wa homoni, hususan za uzazi akisema hazifai.

Pia, anataja chupa za kunyonyeshea maziwa kwa watoto zinashauriwa huko Ulaya, Canada, Uingereza na Australia na Newsealand zisiwe na kemikali ya BPA (BPA free).

Nchini Tanzania, kunashauriwa, endapo mtoto anapewa maziwa, ni vema mzazi, au mlezi atumie kikombe na kijiko, ambacho ni rahisi kukiosha na kukihifadhi.

"Tumia vifungashio vya chupa ya kioo, vyombo vya udongo wakati wa kupasha chakula.

Pamoja na haya kujulikana, bado taka zinaendelea kuhusu matumizi ya chupa za plastiki katika mazingira tulio nayo," anasema Dk. Mzige.

Anafafanua kuwa, tafiti za CDC huko Marekani, Ulaya na Australia, na CDC waliwasiliana wadau John Hopkins kuhusu uvumi kwenye mitandao wakiwanukuu dai la uthibitisho, kuwa maji kwenye chupa za plastiki yakigandishwa na yakikaa juani hayawezi kuleta saratani. Uthibitisho ulikuwa uzushi.

**DIOXIN KEMIKALI HATARISHI**

Dioxin ni kemikali haribifu inayosambaa angani, hewani, na kuingia kwenye maji. Kemikali hiyo ya 'dioxin' hutokea wakati vifaa mbalimbali na uchafu unaozalishwa kwenye viwanda au hospitalini, uchomaji masalia yakehuzalisha 'Dioxin.'

Ng'ombe anaweza kula majani au kunywa maji yaliyochafuliwa na 'dioxin', kuku anaweza kulishwa chakula kilichochafuliwa na 'dioxin' na mayai yakapata athari.

Anasena, samaki baharini, mtoni na maziwa wanakula 'dioxin'. Minofu yao yenye mafuta kwenye miili yao inahifadhi sumu hiyo.

Dk. Mzige, anafafanua kemikali yenye 'dioxin' inapopatikana kwenye nyama inayoliwa kwa muda mrefu, inakaa mwilini na kusababisha saratani za utumbo mpana na aina nyinginezo, za kama tezi dume na saratani ya wanawake.

Anasema, katika chakula cha wanyama wanaoliwa chote kwa ujumla, akitaja asilimia 35 ya saratani zote duniani husababishwa na chakula; pia asilimia 30 ya saratani hizo, zote husababishwa na matumizi ya tumbaku, ugoro, kuberi ndani ya tumbaku na bidhaa zake zote.

Pia, anataja ulaji matunda na mboga za majani, pia kufanya mazoezi ya mwili na viungo, husaidia kuondoa anachokitaja 'atomi na elektroni' haribifu mwilini.

Na kwa hali hiyo husaidia kudhibitu saratani, kisukari, shinikizo la damu na kukupa afya iliyothabitu kimwili na kiakili.

Dk. Mzige anasisitiza watu wazingatie mlo kamili wenye mchanganyiko wa virutubisho ain zote na kupunguza matumizi ya mafuta ya ziada, chumvi na sukari.

Vilevile, kupunguza matumizi yasiyo lazima ya vifaa vya plastiki kuhifadhi, kupikia na kufungashia vyakula.

Ushauri ni kuwa watu wafuate maelekezo ya watengenezaji, wafungashaji na wasindikaji vyakula vinavyoonesha kuacha kuvitumia.

• ***Ni ufafanuzi wake ulipotolewa. Kwa ushauri, wasiliana naye: amzige@hotmail.com.***

# WAINGIA KAZINI KUTEKELEZA MBADALA WA RAIS, KUACHA MKAA ULIOZOELEKA

Inatoka Uk. 11

aweza kununua mkaa lakini usitoshe kupikia vitu vyote, inabidi ukanunue mwingine na kuna wakati ninashindwa!"

Anaeleza kuwa elimu aliyo nayo imekuwa fursa, anayoifafanua kwamba,; "Mkaa mbadala umetusaidia, yaani ukiona karatasi unaokota, watoto daftari wametupa, sijui uchafu gani unaokota unatengeneza mkaa! Yaani hii teknolojia imetusaidia sana, unajikuta unatengeneza mkaa wa kutosha na hauhangaiki tena.'

NISHATI INAVYOUMBWA

Mkufunzi wa Teknolojia hiyo ya mkaa mbadala, kutoka asasi ya Sauti ya Jamii, Kipunguni, Tausi Msangi, anaeleza mkaa huo unatokana na taka tofauti, ukinufaisha uwekaji mazingira safi, huku ikipunguza ukataji miti ovyo uchomaji mkaa misituni.

Anaitaja kuwa teknolojia isiyohitaji mtaji mkubwa na kazi hiyo inaweza kufanyika majumbani, ubunifu ulioasisiwa ughaibuni miaka kadhaa iliyopita, akiitaja nchi jirani Kenya imeanza kuitumia mapema.

Tausi anataja malighafi yanayoohitajika katika kutengeneza mkaa mbadala, ni pamoja na vumbi la mkaa wa kawaida linalopatikana maeneo yao ya biashara.

"Unaweza kulipata bure au kulinunua kwa gharama ndogo halafu ukatumia gundi ya udongo unaonatanata kama ule ambao unatumika kutengenezea tofali za kuchoma na vyungu, unaweza pia kutumia uji wa muhogo kutengeneza mkaa huo," anaeleza Tausi.

Malighafi mengine anayataja ni maganda ya machungwa yaliyokatwa vipande vidogo, yanakaushwa na kulowekwa maji kwa muda wa siku mbili au tatu.

"Kwa mfano, unaweza kuchukua vumbi lako la mkaa ambalo halina mabonge na kama yapo unatafuta mfuko ukaweka ndani halafu, ukatwanga mpaka yalainike kabisa, ukachekecha kuondoa mabonge ambayo yamebakia," anasema.

"Tunachokihitaji hapa ni ule ungaunga 'mlaini' peke yake, kisha uweke kwenye chombo kama vile beseni au ndoo," anaeleza na kuongeza:

"Baada ya hapo unatakiwa uchukue udongo mkavu ambao uko katika hali ya ungaunga, kama una mabonge utwange mpaka ulainike, kisha uchanganyie katika lile vumbi la mkaa mpaka vumbi la mkaa na udongo vichanganyike kabisa.

"Weka gundi katika huo mchanganyiko au ongeza maji ikiwa udongo umetumika kama gundi, halafu changanya hadi uridhike vyote kwamba vimechanganyikana vizuri."

Tausi anaeleza baada ya kuvichanganya, huzalisha mkaa, anaoufafanua: "Unaweza kutumia mkono kwa kutengeneza muundo unaoupenda kama vile vitonge.

'Wakati wa kutengeneza muundo huo, hakikisha unabinya kwa nguvu ili ziwe ngumu kwani kadri unavyokuwa mgumu ndivyo itakavyotengeneza mkaa mzuri zaidi."

Anasema baada ya mtu kutengeneza muundo unaoutaka kulingana na jiko lake, hatua nyingine inaanikwa juani wastani wa siku mbili au tatu, ikauke tayari kwa matumizi.

AFYA

## MAAJABU KISUKARI CHA MBUNGE...

# Dk. Malima aligundua kwa simu, Janabi akaendeleza safarini Hijja

## •Leo? Katoka hali hatari, hadi hatumii dawa

**Na Christina Mwakangale**



Mbunge wa Mbagala, Abdallah Chaurembo. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE.**



Dk. Amani Malima; aliyemgundua mbunge ana tatizo kubwa, 'akamlaza' siku tatu.

KIAFYA, Mbunge wa Jimbo la Mbagala, Abdallah Chaurembo, leo hii anasimama kuwa shujaa wa ugonjwa wa kisukari.

Kisukari hasa cha aina ya pili, ni miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza (NCDs), ambayo chanzo chake kinatajwa kuwa ni mtindo wa maisha.

Chaurembo, ana simulizi yake kuhusu ugonjwa huo, akifafanua kwa hatua namna alivyoanza kuumwa, kufikia matibabu na safari ya Hija huko Mekka, kulivyobadili mtindo wake wa maisha.

Prof. Mohamed Janabi, mwanataaluma, tabibu na bingwa aliyebobea kwenye magonjwa yaliyomo kwenye kundi la NCDs, katika kitabu chake cha 'Mtindo wa Maisha na Afya Yako', anamuelezea baada ya kukutana na mbunge huyo huko Mekka, akimpa mbinu na tiba lishe ambayo Chaurembo anaitumia hadi sasa.

Msomi huyo wa afya, anaeleza zamani matibabu ya kisukari yalikuwa ni mgonjwa akishaanza kutumia dawa za kisukari, ataendelea na utaratibu huo maisha yote.

"Lakini kuanzia mwaka 2021, imekuja kugundulika kwamba uzito ukipungua na masharti yote yakifuatwa, kuna uwezekano wa mgonjwa kuachana na dawa na badala yake akawa anazingatia zaidi mtindo wa ulaji," anasema Prof. Janabi.

### SIMULIZI YA CHAUREMBO

Abdallah Chaurenbo anasimulia madhila ya ugonjwa huo, akitoa ushuhuda kwamba inawezekana kuachana na dawa za kisukari na masharti ya ulaji chakula yakazingatiwa sawasawa.

Aidha, anasema kwamba, mara ya kwanza kugundua kwamba anaugua kisukari ilikuwa mwaka 2010.

Anakumbukua kwamba ilikuwa ni majira ya saa 11 jioni akajikuta kila baada ya dakika 10 anakwenda haja ndogo.

Hatua ya kwanza aliyoichukua, ni kumpigia simu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Temeke, Amani Malima na kumweleza hali aliyokuwa nayo.

Dk. Malima akamtaka atafute hospitali iliyokuwa karibu naye akapime sukari. Anasema alipata mahali pa kupima zahanati iliyokuwa jirani na kipimo kilionyesha kuwa sukari iko 35.8.

Baada ya muda Dk. Malima alimtafuta kujua anaendeleaje na kipimo kinasemaje. Chaurembo alimpa taarifa kuhusu kipimo. Taarifa hizo zilimshitua Dk. Malima na alimtaka aende Hospitali ya Temeke mara moja.

Hata hivyo, Chaurembo hakujishughulisha, kwa kuwa hakujua kwa kina madhara ya kisukari

Chaurembo anasimulia kwamba, Dk. Malima aliendelea kumpigia simu na mwishowe aliamua kumfuata mwenyewe nyumbani kwa gari la kubeba wagonjwa na kumpeleka hadi hospitalini.

Alipofika hospitalini Temeke, alimpima tena sukari na kukuta ikiwa 32.5. Alilazwa na kuwekewa dripu kwa siku tatu akiwa na fahamu. Baadaye sukari ilishuka mpaka 12 ndipo aliporuhusiwa kurejea nyumbani. Hapo aliishauriwa atafute mtaalamu wa kisukari, ili amsaidie kujua jinsi ya kuishi na ugonjwa huo.

Chaurembo, aliendelea na maisha akipata matibabu 'hapa na pale', mpaka alipokutana na Prof. Mohamed Janabi mwaka 2012 walipokuwa wamekwenda Hija Mekka.

Hata hivyo, wakiwa Mekka alipima sukari ikawa 22, ndipo alipopata fursa ya kumsikia Prof. Janabi kuhusu ugonjwa wa kisukari.

Anasimulia kwamba Prof. Janabi alimatahadharisha kwamba kisukari ni ugonjwa hatari, lakini mtu anaweza kuudhibiti.

Hata hivyo, anasema akammpa angalizo kwamba dawa za kisukari zilizopo ni za kushusha sukari, sio kumaliza tatizo.

"Jambo kubwa la kufanya ili kukabiliana na kisukari ni kubadili mtindo wa maisha. Kama mgonjwa wa kisukari hatabadili mtindo wa maisha katika ulaji wa chakula, atatumia dawa hizo milele," akamwambia mbunge huyo.

Akamuongezea kwamba kama mgonjwa akifuata masharti ya wataalamu, anaweza kuacha kabisa dawa wakijadiliana na daktari wake akimtaka kitaalamu 'it's a reversible disease'.

Chaurembo anaeleza katika siku 21 walizokaa huko Mekka, Prof. Janabi alimsaidia sana kujua ale chakula gani na muda gani, pamoja na muda wa kufanya mazoezi, ili kukabiliana na sukari mwilini.

Baada ya kumaliza Hija, Prof. Janabi alisema afike anakotibu, yaani Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ili waone jinsi anavyoweza kuendelea kuishi na kisukari.

Hata hivyo, anasema baada ya kurudi nchini aliendelea na shughuli zake na hakwenda kumuona, mpaka Prof. Janabi alipomtafuta na kumkumbusha kuhusu miadi yao ya kukutana kwa kumsisitiza ufuatiliaji wa karibu, kabla ya kusimamisha matumizi ya dawa kabisa.

### MWANZO WA MASHARTI

Chaurembo anasimulia kwamba, Prof. Janabi, alimtaka mbunge huyo aende na familia yake mahali hapo, jambo ambalo Chaurembo alitii, akichukua wake zake wawili na watoto wakaenda kumwona Prof. Janabi

Kwa pamoja aliwafundisha kwamba, daktari na kliniki ya kwanza ya mgonjwa wa kisukari ni familia na akawauliza wanapata faida gani kwa baba yao (Chaurembo), mume wao akiwako na walijieleza kuwa huduma anawapatia kama vile nguo, pesa za matumizi na mambo mengine.

Prof. Janabi aliwaeleza kwamba ugonjwa wa kisukari una masharti ya kuishi nao na ni hakika kama yasipofuatwa, mgonjwa anaweza akapunguza uhai wake.

Aliwaambia wanafamilia hao kwamba wasipofuata masharti watampoteza baba au mume wao.

Pia, Chaurembo, alipewa masharti ya chakula ambacho mgonjwa wa kisukari kinamfaa, kikubwa ni kukaa mbali na lishe ya wanga ana akamtaka kuwa na kipimo cha sukari.

Akawashauri, wasile vyakula vya wanga nyumbani wakati Chaurembo akiwapo, kwamba ni hali itamsaidia kutokutamani na mwishowe hatokula.

Chaurembo anasimulia kwamba, vyakula vya wanga akiwa nyumbani vinaliwa kwa kificho, yeye kwake vinatawala ni 'mbogamboga', samaki, bamia, mlenda, ndizi bokoboko zikiwa mbichi tena changa na mtori kidogo.

Kutokana na kuendelea kupima sukari kila wakati, mkewe alimshauri kwamba kuna uwezekano wa kujikuta katika shinikizo kutokana na utaratibu wa kujipima kila wakati.

Badala yake, Prof. Janabi alimshauri ajenge tabia ya kujisikiliza mwill ili kugundua vitu ambavyo vikitokea atajua sukari mwilini haiko sawa.

Muda wote Prof. Janabi alisisitiza kwamba tutibu kisukari na siyo sukari kwa lugha yake "lets treat diabetes, not controlling sugar.'

### CHAUREMBO ANAVYOJITAMBUA:

Chaurembo anasema dalili kama Kuna hitilafu ni kupata haja ndogo kila mara, koo kukauka (kiu), kuhisi ganzi; na mwili kuwaka moto.

Kwa kuwa shughuli zake nyingi za kiuchumi alikuwa anafanya mkoani Lindi na kuhudhuria Bunge, Jijini Dodoma, alipanga ratiba zake kwamba, akiwa safarini kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma bungeni, akienda haja ndogo mara moja ndani ya saa nane, anajua sukari yake iko vyema,

Akisafiri kati ya Dar es Salaam na Lindi, akienda haja ndogo mara moja, hapo anatambua sukari iko sawa;

Vilevile anasema, usiku inapomtokea analala na kuamka kwenda haja ndogo zaidi ya mara mbili, atajua sukari yake haiko sawa mwilini na

Akienda mara moja au kutokwenda kabisa usiku kucha, atajua kuwa sukari iko sawa.

Chaurembo anatoa ushahidi kwamba, mgonjwa wa kisukari akifuata masharti, hana sababu ya kutumia dawa. Anasema kwa sasa sukari yake huwa kati ya 4.7 ama 5.8, kiwango ambacho ni cha kawaida.

Hata hivyo, anatoa angalizo kwamba kuna wakati inakuwa 5.7, lakini baada ya kula inashuka zaidi hadi 4.5.

Baada ya kuzungumza na wataalamu wa tiba, aliambiwa kwamba asiache kabisa kula wanga, ila azingatie anakula saa ngapi na kwa kiasi gani. Hiyo, ni kutokana na ukwel mwili unahitaji wanga, ili uweze kujiendesha,

### SOMO LA MUDA

Chaurembo anasema kuwa mtu akila wanga saa moja usiku, analala ni kuzalisha sukari.

Binafsi, yeye huwa anakula wanga kama ugali au wali saa nne asubuhi, kisha anaenda kwenye shughuli zake za kila siku.

Jioni huwa anakula matango, parachichi na mboga au ndizi mbichi za kuchemsha.

Vilevile, anaserma ingawa wapo matabibu wanashauri watu kula wanga (kama wali) sawa na ukubwa wa ngumi zao, kwake ilikuwa vigumu kwani ilionekana kuwa ni kiasi kikubwa kingesababisha kuibuka kwa sukari,

Yeye anaweka konzi moja ya wanga kisha anakula na samaki mkubwa, matunda mboga za majani kama matembele na mchicha.

Chaurembo anashauri kwamba,

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Zahanati inayonusuru safari ya Km. 14, tiba usiku iko kwa tochi

**Na Shaban Njia, NGARA**

HUKO nyuma kihistoria, wakazi wa kijiji cha Rwakaremera katika kata ya Kasulo wilayani Ngara mkoani Kagera, hali ilikuwa mbaya kufikia huduma ya afya.

Walikuwa nyuma na maisha ya kutumia Sera ya Afya ya Mwaka 2017, inayotaka kila kijiji kuwa na zahanati, kata kuwa na kituo cha afya, wilaya hospitali, pia mkoa kuwa na hospitali ya rufani.

Ni madhila yaliyowafikisha kuchangishana kila kaya Sh.20,000 na zikapatikana Sh. milioni 30, wakaanzisha ujenzi mwaka huo 2021 hadi kufikia boma na baadaye serikali ikatoa Sh. milioni 50 za ukamilishaji, kazi iliyotimia mwaka 2022 na kuanza kutolewa huduma za tiba.

Hata hivyo, kukaibuka changamoto nyingine ya kukosekana nishati umeme katika zahanati, sasa ikidumu miaka mitatu hata ikabaki kwa dharura ya mgonjwa usiku pekee.

Inapotokea, watendaji wanalazimika kutumia tochi ya mlinzi au simu ya mtoa huduma wa zamu usiku, ndio chanzo cha mwanga, jambo linalowanyima amani na sasa wanaiangukia serikali kuharakisha utatuzi wake wa umeme unaojitosheleza.



Zahanati ya Kijiji Mwakarebera, Kata ya Kasulo, wilayani Ngara mkoani Kagera. Juu yake ni umeme wa jua unaotumika kuhifadhi dawa na chanjo kwenye friji. **PICHA: SHABAN NJIA.**

Hiyo inachukua nafasi sasa, huku kukitajwa kitakwimu ujenzi huo umesaidia kuongeza idadi ya wagonjwa wa nje (OPD) wanaofika kupata huduma wakiwa 42,252,741 mwaka jana, kwa mujibu wa ripoti za ziara za kiafya; kutoka 41,347,690 mwaka 2022. Ni ongezeko la wagonjwa 905,501.

Katika idadi hiyo, waliopata huduma ngazi ya zahanati walikuwa asilimia 33, wenye rufani vituo vya afya asilimia 18, hospitali za halmashauri asilimia 23, asilimia tisa, Kanda na Taifa asilimia 17.

John Nkwale, mlinzi wa zahanati hiyo anaeleza namna amekuwa akiitumia tochi yake usiku kuwa msaada kwa wagonjwa wa dharura usiku na kikwazo hicho kimewafanya baadhi ya wagonjwa kwenda vituo jirani.

"Zahanati haina umeme, isipotumika simu za watoa huduma basi jua tochi yangu itatumika kama mwanga..." anaongeza Nkwale.

**MGANGA MFAWIDHI**

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, John Samwel, anakiri hali hiyo, hata wanatoa huduma mchana pekee na usiku hakuna mjamzito walishampokea, zaidi ya wagonjwa wa kawaida.

Anasema, kila katika kliniki za wajawazito, wamekuwa wakiwasisitiza kuhifadhi fedha za dharura kila wanapokaribia kujifungua, waweze kusafiri mpaka hospitali jirani za Lukole, Kasulo na Nyamiaga kupata huduma ya uzazi.

Dk. Samwel anasema kwa mwezi mmoja, wajawazito wanaofika kupata huduma kwake ni kati ya 30 mpaka 50 na kuna mwezi idadi ilishafika 80, huku malengo waliyopewa wagonjwa wasishuke chini ya 15, hivyo kituo kinahitajka kuongezwa ukubwa hasa upande wa kliniki.

Anafafanua kuwa, kituo kina mabenchi sita, mawili kati yake yanatumiwa na wagonjwa wa nje na manne wanatumia wajawazito wanaofika kliniki na kuna wakati wanalazimika kukaa chini ya miti inayozunguka zahanati.

Dk. Samweli anasema, zahanati ina umeme wa jua (Sola), lakini unatumika kuhifadhi dawa na vitu kwenye friji tu na hautakiwi kutumika kwenye vyumba vingine, ndio sababu ya kukosa umeme.

Anasema awali alishirikisha serikali ya kijiji kuangalia namna ya kufikisha umeme na zilitakiwa nguzo mbili kwa Sh.600,000, kutoka kwenye chanzo kikuu, lakini ulipofanyika upembuzi yakinifu awamu nyingine, zilihitajika nguzo nne kwa Sh. milioni nne, zilikwishalipwa TANESCO kuleta umeme.

Dk. Samwel anafafanua kuwa zahanati ilishindwa kufikisha umeme kwa sababu mapato yao yameelekezwa kwenye matumizi mengine kama kununua dawa, hivyo wakachukua hatua kuomba msaada wilayani kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, sasa muda wowote umeme utapatikana.

**UONGOZI KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Rwakaremera, Jonathan Zofilo, anasema kukosekana nishati hiyo imebaki kikwazo kwa watoa huduma na wagonjwa zahanati husika, akihimiza kutafutwa suluhisho haraka kuepuka anachokiita 'watajifungulia gizani.'

Diwani wa Kata ya Kasulo Yusufu Katura, anasema awali kila mwezi wajawazito watano mpaka nane walijifungulia njiani wakienda Kituo cha Afya Lukole, umbali wa kilomita 14 kutoka kijijini hapo au Hospitali ya Nyamiaga kilomita 45. Hata hivyo, jema hakuna vifo vilivyojitokeza.

**WANANCHI KASULO**

Christina Julius, mkazi wa kitongoji cha Njiapanda, anasema, lengo la kujenga na kusogeza huduma karibu ilikuwa kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu na kukabili dharura za kitabibu, kwani walishayona madhara, hasa kwa wajawazito na watoto wachanga.

"Mwaka 2018 ndugu yangu aliwahi kujifungulia njiani akielekea kituo cha afya Lukole kujifungua, nilishuhudia adha alizopata na 'Mungu saidia' alijifungua salama, ila tulimsaidia.

"Tulikuwa naye na watu waliokuwa wakipita njia! Nilipoambiwa suala la kuchangia ujenzi wa zahanati, sikusita kwa sababu umuhimu wake naufahamu," anasema Christina. Aniceth Andrew, anayeishi kitongoji cha Nguvukazi, anasema siku za kliniki zao wamekuwa wakikumbushwa kujiandaa kwa fedha za usafiri kwenda hospitali kupata huduma, kwani inapotokea anapata uchungu usiku, hawezi kupata huduma zahanati kwa sababu ya kukosekana umeme.

"Wajawazito wanahudhuria tu kliniki ili kujua maendeleo ya watoto wao tumboni, inapofika muda wa kujifungua tunalazimika kuwasafirisha mpaka Hospitali ya Nyamiaga kilometa 35 mpaka 40 au Kituo cha Afya Lukole, kilometa 14, wapo tunaokutana nao wamejifungua njiani," anasema Andrew.

Anasema, ni kawaida kliniki zote za wajawazito wanasisitizwa kuhifadhi fedha za dharura, anapokaribia kujifungua, asafiri mpaka hospitali jirani kama ya Lukole.

## DK. MALIMA ALIGUNDUA KWA SIMU, JANABI AKAENDELEZA SAFARINI

**Inatoka Uk. 13**

ni vyema kujiepusha na vyakula vya sukari, kwani madhara yake mwilini ni makubwa, kama kusababisha ugonjwa wa kisukari ambao nao husababisha magonjwa kama ya figo, ambayo matibabu yake ni ghali sana. Anawashauri watu wanaoishi na wagonjwa wa kisukari, kuepuka kula mbele yao vyakula walivyokatazwa, kwani watawatamanisha na mwishowe nao watakula, hivyo kujiongezea matatizo ya ugonjwa huo.

"Mwisho, nashauri wagonjwa wa kisukari kuacha kutumia dawa za meno zenye utamu na badala yake watumie zenye chumvi chumvi na pilipili."

**NJIA KUEPUKA NCDs**

Prof. Janabi katika kitabu hicho anasema, ni vyema ikajulikana wazi njia ya kujiepusha na magonjwa hayo ni rahisi na isiyokuwa na gharama.

Kikubwa zaidi anataka, ni kuepuka magonjwa hayo na mtu anapata faida na nafuu kubwa ya maisha. Kwa hiyo watu wanashauriwa wafanye yafuatayo:

Kubadili mtindo wa maisha kuhusu ulaji: Chagua unakula chakula gani; tambua unakula saa ngapi; fanya mazoezi, walau tembea hatua 10,000 kwa siku.

Bingwa huyo anasema pia kuepuka ponbe na kuacha kuvuta sigara ni muhimu.



## HABARI DODOMA

# Wanafunzi 198,986 wadahiliwa masomo ya shahada

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA mwaka wa masomo 2024 Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imedahili wanafunzi wa shahada ya kwanza 198,986, ikilinganishwa na wanafunzi 186,289 katika mwaka wa masomo 2023.

Pia, programu zimeongezeka kutoka 809 mwaka 2023/24 hadi 856 kwa mwaka 2024/25, ikiwa ni ongezeko la programu 47.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu udahili wa wanafunzi wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Alisema katika awamu ya kwanza ya udahili waombaji walikuwa 124,286 wakiwa wametuma maombi ya kujiunga na vyuo 86 vilivyoidhinishwa kudahili wanafunzi katika shahada ya kwanza.

Aidha, alisema katika awamu ya kwanza ya udahili jumla ya waombaji 98,890 sawa na asilimia 79.6 ya waombaji wote walioomba wamepata vyuo.

Hata hivyo, alisema idadi ya waombaji wa udahili inatarajia kuongezeka katika awamu ya pili ambayo imetangazwa kwa ajili ya wanafunzi weye sifa kuomba katika vyuo mbalimbali nchini.

> **"Kwa kuzingatia kuwa, mabwawa pamoja na kuwa ni miundombinu muhimu kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa shughuli za kiuchumi na kuhifadhi tope sumu litokanalo na shughuli...**

Alisema, awamu ya pili ya udahili imeanza jana, itakwenda hadi Septemba 21, huku akiwasisitiza wanafunzi kutumia muda huo kuomba nafasi ili waweze kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Hata hivyo , alisema waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja wanapaswa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimoja ambacho anatarajia kwenda.

Alisema, uthibitisho huo utafanyika kwa kutumia namba maalum ya siri iliotumwa kwa ujumbe mfupi kwenye namba zao za simu au barua pepe wakati wa kuomba udahili.

Alisema, wale ambao hawajapata kwa wakati ujumbe huo wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo wakudahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

"Waombaji wa shahada ya kwanza wanakumbushwa kuwa, masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika" alisema.

Aidha, alitoa wito kwa wanafunzi kuchangamkia fursa za udahili ambazo zimetolewa kwa awamu ya pili ili waweze kupata nafasi za masomo ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.



Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la AMREF Tanzania, Dk. Florence Temu (kulia), akitoa elimu ya jinsi ya kuandaa andiko la miradi kwa wadau wa asasi za kijamii wakati wa mkutano wa jukwaa la mwaka la mashirika yasiyo ya kiserikali, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watanzania changamkieni fursa za kusoma Finland

**Na Faustine Feliciane**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa ya kusoma bure nchini Finland ili kuandaa 'diaspora' watakaokuwa na moyo wa kuwekeza nchini.

Mwanzilishi mwenza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya ExamNet Tanzania, Rodgers Mbaga alisema hayo jana jijini Dar es Salaam.

Taasisi hiyo ni wakala rasmi wa Taasisi ya Finest Future ya Finland inayosaidia kuwapatia vijana kutoka Afrika fursa kupata nafasi za kusoma bure nchini humo, alisema jana.

"Umeanzishwa mpango maalum na Taasisi ya Finest Future ya kuwapa nafasi vijana kupata elimu Finland, mpango huu unahusisha nchi mbalimbali kutoka Afrika na Asia, kwetu Tanzania tunawahimiza vijana wenye sifa kujitokeza kuomba nafasi hii ambayo itawasaidia kusoma bure nchini humo kupitia taasisi hiyo," alisema Mbaga.

Alisema kigezo kikubwa cha kupata nafasi hiyo ni kujifunza lugha ya Kifin inayotumiwa nchini humo na baada ya kusoma kwa kipindi cha miezi 18 wakiwa hapa nchini watapata fursa hiyo.

"Tukiwa na vijana wengi wanaosoma nje itasaidia kupata 'diaspora' ambao baadaye watakuja kuwekeza Tanzania na kuunga mkono juhudi za serikali za kuwaahimiza Watanzania waliopo nje ya nchi waje kwa wingi nchini kuwekeza," alisema.

Alisema mwanzilishi na Mkurugenzi wa Finest Future, Peter Vesterbacka, kutoka Finland anatarajiwa kuwapo nchini kwenye tamasha kubwa la masuala ya elimu litakalofanyika Jumamosi ijayo, jijini Dar es Salaam.

"Kwenye tamasha hili maalum, wazazi watapata fursa ya kuuliza maswali juu ya programu hii, huku pia wakiwasikia wanafunzi ambao wamepata nafasi ya kwenda kusoma Finland, kutakuwa na mahojiano ya moja kwa moja na wanafunzi hao kutoka nchini humo," alisema Mbaga.

Aidha, alisema tamasha hilo litafanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kijitonyama.

# Watendaji miji, wilaya wapewa elimu Sheria ya Ununuzi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KUTOKUWAPO kwa uelewa kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura Namba 410, Wizara ya Fedha imeanza kutoa mafunzo kwa watendaji wa serikali waliopo katika ngazi za mikoa, halmashauri za majiji, miji na wilaya.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo alisema hayo jana wakati wa hotuba yake katika mkutano unaohusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura na. 410, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura Na. 103 na mafunzo ya matumizi ya takwimu zinazozalishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu uliofanyika jijini hapa.

Omolo alisema matatizo mbalimbali yanayohusu Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na matumizi sahihi ya takwimu zinazoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imesababisha kuanza utaratibu huo wa kutoa elimu kwa viongozi wa ngazi hizo.

"Watendaji waliopo hapa wanashiriki wakiwa ni wawakilishi wa watendaji wote walio katika taasisi wanazotoka kupitia washiriki hawa, tunategemea watakuwa chachu ya kuwafundisha watendaji wengine katika taasisi wanazozitumikia.

Alisema mkutano huo unahusisha mawasilisho ya mada tatu mada hizo zinahusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023, Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na matumizi sahihi ya takwimu.

Omolo alisema mada ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ina lengo la kuwafahamisha Watanzania juu ya fursa mbalimbali zinazopatikana katika sheria hiyo.

Alitaja fursa hizo ni kama upendeleo wa makundi mbalimbali ya jamii, upendeleo kwa wataalamu na kampuni za ndani, matumizi ya rasilimali zinazozalishwa au kuchimbwa hapa nchini katika utengenezaji wa bidhaa.

Aidha, alisema kupitia mawasilisho haya, wanatarajia kuibua mijadala mbalimbali itakayopelekea maazimio yatakayotumika kuandaa mikakati ambayo utekelezwaji wake utaongeza matumizi ya fursa zilizowekwa kisheria kupitia sheria hizo.

Alisema kwa upande wa matumizi ya takwimu sahihi, utekelezwaji wa mikakati itakayowekwa, utaongeza uhalisia wa maandalizi ya mipango mbalimbali ya serikali ambayo itahitimishwa kwa kupatikana kwa huduma bora kwa watanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule aliwashukuru wizara hiyo kwa kuandaa semina ambazo zitasaidia kuwafikia wananchi katika kunufaika na sheria hiyo ya manunuzi.



# Wajasiriamali 62,000 kusajiliwa kidijitali, kuwezeshwa kiuchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJASIRIAMALI zaidi ya 62,000 wanatarajiwa kusajiliwa kwenye mfumo rasmi wa kidijitali na kuwezeshwa kiuchumi kupitia Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) iliyoanzishwa hivi karibuni na serikali.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Bang'i Issa, aliyasema hayo juzi mkoani Mbeya wakati wa kikao kazi na viongozi wa serikali kilichokuwa na lengo la kuitambulisha programu hiyo kimkoa.

Kikao hicho kiliwahusisha viongozi wa NEEC wa Mkoa wa Mbeya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na wajasiriamali wa maeneo mbalimbali ya mkoa huo. Alisema programu hiyo ya IMASA, inalenga kuwawezesha kiuchumi wananchi wa makundi maalumu hasa vijana, wanawake na wazee na watu wenye ulemavu ambao wako kwenye vikundi vya uzalishaji kulingana na eneo lao.

Alisema kabla ya kuanza kutekeleza programu hiyo wanafanya tathmini ya hali ya uchumi wa wananchi kuanzia katika ngazi ya vitongoji, vijiji na mitaa na kuanza kurasimisha ardhi, bidhaa zinazozalishwa na wananchi kwa kuzingatia mwongozo maalumu wa kitaifa. "Tunaonana na ninyi viongozi kwa sababu nyie ndiyo wasimamizi wa programu hii huku chini, serikali haiwezi kumwinua kiuchumi mwananchi mmoja mmoja, ndiyo maana imeanzisha hii programu ambayo inalenga kuwawezesha wananchi katika makundi," alisema Bang'i.

Alisema programu hiyo imeshatambulishwa katika mikoa 13 nchini na Mkoa wa Mbeya ni wa 14 na kwamba baada ya kuhitimisha Mbeya wataendelea katika mikoa mingine.

Baadhi ya viongozi walioshiriki kikao hicho waliishukuru serikali kwa kuanzisha programu ya IMASA wakisema itasaidia kuinua uchumi wa wananchi hasa wajasiriamali.

Mwenyekiti wa NEEC Mkoa wa Mbeya, Neema Kisanga, alisema wananchi wengi mkoani humo hasa wanawake wamekuwa wakipambana kufanya biashara mbalimbali ili kujiinua kiuchumi lakini wamekuwa wakikosa mitaji.

Alisema kupitia programu hiyo, watapata mitaji ambayo itawasaidia kuendesha biashara hizo pamoja na kujiinua kiuchumi, huku akidai kuwa wanufaika watapata pia elimu ya uendeshaji wa shughuli zao.

"Ukienda kwa wanawake huko mitaani unakuta wana mawazo mazuri sana ya kuendesha biashara, lakini wanashindwa kutembea kwenye mawazo hayo kwa sababu ya kukosa mitaji, tunamshukuru Rais Samia kwa kuanzisha programu hii," alisema Neema.

Mmoja wa wajasiriamali walioshiriki kikao hicho, Everine Kanei ambaye ni mmoja wa wanachama wa kikundi cha uchakataji na uuzaji wa maziwa kutoka Kijiji cha Mtebete wilayani Mbarali alisema programu hiyo itawasaidia kuboresha mifugo yao.

Alisema watapata fedha kwa ajili ya kununua vyakula na madini mbalimbali kwa ajili ya mifugo na hivyo kuongeza uzalishaji wa maziwa kufikia lita 20 kwa kila ng'ombe.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Katibu Tawala wa Mkoa huo, Lodrick Mpogolo aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kusimamia uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi katika maeneo yao ili kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema kwa mujibu wa mwongozo wa programu hiyo, vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi ni lazima vianzishwe jirani na maeneo ya uzalishaji ya wananchi. Alisema kila wilaya katika mkoa huo ina vipaumbele ambavyo programu hiyo itawasaidia wananchi kulingana na uzalishaji wanaoufanya kwenye eneo lao.

Alisema katika Wilaya ya Chunya kuna uchimbaji wa dhahabu, kilimo cha mpunga wilayani Mbarali, kilimo cha kakao wilayani Kyela, kilimo cha pareto katika Wilaya ya Mbeya, kilimo cha ndizi katika Wilaya ya Rungwe na biashara na usindikaji katika Jiji la Mbeya.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (kushoto), akimsikiliza mmoja wa wafanyabiashara wa Soko la Makongolosi, wilayani Chunya juzi, alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama hicho, hasa katika uboreshaji wa miundombinu. **PICHA: NEBART**

# Zimamoto: Leteni ramani tuzihakiki kabla ya ujenzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kupeleka ramani za nyumba zao katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla ya kuanza kujenga ili washauriwe namna ya kukabiliana na majanga ya moto yanayoweza kuibuka.

Kamanda wa Jeshi hilo Mkoa wa Mbeya, Mratibu wa Zimamoto, Malumbo Ngata alisema majanga mengi ya moto yamekuwa yakitokea na kuteketeza makazi ya watu na mali zilizomo kutokana na ujenzi holela ambao hauzingatii kinga ya moto.

Alisema kwa mujibu wa sharia, kila mwananchi anatakiwa kupeleka ramani kwa jeshi hilo kabla ya kujenga ili ashauriwe namna sahihi ya kujenga nyumba kwa kuzingatia kinga dhidi ya majanga ya moto.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo tofauti ili kuhakikisha kila mmoja anakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kukabiliana na majanga ya moto, ili kupunguza madhara.

Alisema wanatoa elimu hiyo kwa makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo wanafunzi wa shule za sekondari na msingi ili kuwaandaa watoto hao kuwa na uelewa wa kukabiliana na majanga hayo.

Alisema kwenye maeneo yote ya mikusanyiko ya watu, maofisa wa jeshi hilo wamekuwa wakitoa elimu na kuhakikisha vifaa vya kukabiliana na moto vinakuwapo vya kutosha.

# H'shauri yaanza ukarabati wa Soko la Makongolosi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imeanza utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kuboresha miundombinu ya Soko la Makongolosi wilayani humo, ambalo lilikuwa linahatarisha maisha ya wafanyabiashara na wateja wao.

Februari mwaka huu, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alifanya ziara katika soko hilo ambapo wananchi waliibua kero mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa choo, gari la kuzoa taka na paa kuvuja wakati wa mvua.

Kutokana na hali hiyo aliagiza halmashauri hiyo kutenga bajeti kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya soko hilo ili kuwaepusha wananchi na madhara ikiwamo magonjwa ya mlipuko.

Juzi kiongozi huyo wa CCM alifanya ziara ya kushtukiza katika soko hilo kwa lengo la kukagua utekelezaji wa maagizo yake na kukuta yameanza kutekelezwa kwa awamu mbalimbali, hasa ununuzi wa gari la kuzoa taka na ujenzi wa choo.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi, Linus Mwanitega, alisema halmashauri imetenga Sh. milioni 48 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la soko hilo pamoja na ujenzi wa soko jipya la matunda.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 40 ni kwa ajili ya ujenzi wa soko la matunda na Sh. milioni nane ni kwa ajili ya ukarabati wa jengo la zamani ambalo limekuwa likivuja katika baadhi ya maeneo. Vilevile, alisema mpaka sasa wameshaanza kujenga choo cha kisasa katika soko hilo ambalo awali wananchi walikuwa wanatumia cha zamani kilichokuwa na matundu manne pekee ambayo yalikuwa hayakidhi mahitaji. Baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo waliishukuru serikali kwa kuanza utekelezaji wa maagizo hayo wakidai kuwa, soko lao lilikuwa na hali mbaya na lilikuwa linatishia usalama wa afya zao. Mmoja wa wafanyabiashara hao, Falisa Sanga, alisema walikuwa wanatozwa fedha nyingi na vijana ambao walikuwa wanawasaidia kuzoa taka hali ambayo ilikuwa inawasababishia kero na kutoamini serikali.

Alisema tangu MNEC Mwaselela alipotoa maagizo ya kuboresha soko hilo walianza kuona mabadiliko hasa viongozi kuanza kukagua na kuanza kuwashirikisha namna ya kuboresha baadhi ya maeneo.

Mwaselela alisema chama hicho kitaendelea kufuatilia uboreshaji wa soko hilo pamoja na maagizo mengine ambayo kilitoa ili wananchi wapate wanachostahili.

Aliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali wilayani humo ikiwamo ujenzi wa kituo cha mabasi ambacho kimeidhinishiwa Sh. milioni 750 na kuidhinisha Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya afya hasa ununuzi wa vifaa tiba.

HABARI ZANZIBAR

## Dk. Mwinyi: Mauzo Tanzania, Indonesia yaongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ongezeko la thamani ya mauzo ya nje kutoka Tanzania kwenda Indonesia yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 13.53 mwaka 2019 hadi Dola milioni 33.77 mwaka 2023.

Amesema bidhaa kuu za Tanzania zinazouzwa nchini Indonesia ni pamoja na tumbaku, kakao, maharage, karanga, karafuu, pamba na mafuta ya mawese.

Dk. Mwinyi alisema Tanzania na Indonesia zinaadhimisha miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia mwaka huu, kwamba nchi hizo mbili zinajivunia urafiki uliodumu na unaoendelea kukua siku hadi siku.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika mwendelezo wa siku ya pili ya Jukwaa la Indonesia na Afrika 2024 lililofanyika nchini Indonesia.

Dk. Mwinyi katika jukwaa hilo amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema Tanzania bado ina fursa nyingi za uwekezaji ikiwamo kilimo, madini, utalii, na uchimbaji wa mafuta na gesi na uchumi wa bluu. Hivyo, aliwakaribisha wawekezaji kutoka Indonesia kuja Tanzania kuzifanyia kazi fursa hizo.

Kuhusu elimu, Dk. Mwinyi alishukuru serikali ya Indonesia kwa kuendelea kuiunga mkono Tanzania katika sekta ya maendeleo ya rasilimali watu kupitia udhamini wa masomo ya muda mfupi na muda mrefu katika nyanja mbalimbali.

Pia, alitaka Serikali ya Indonesia iongeze udhamini wa masomo pamoja na kubadilishana uzoefu katika maeneo mbalimbali kama vile huduma za afya na sayansi ya tiba, uhandisi, ICT, uvuvi, utalii, ufugaji wa samaki na ilimo.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi alishuhudia utiaji saini wa makubaliano ya udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kushirikiano katika usajili wa bidhaa hizo, ukaguzi pamoja na kupeana taarifa za madhara ya dawa na vifaa tiba kwenye masoko.

Katika hafla hiyo Tanzania iliwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu Dk. Adam Fimbo kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi Tanzania (TMDA), na kwa niaba ya Serikali ya Indonesia iliwakilishwa na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Chakula Indonesia (BPOM) Dk. Taruna Ikrar.

Aidha, Dk. Mwinyi amewasilisha salamu kutoka Rais Samia Suluhu Hassan kwa viongozi wa juu wa mataifa mbalimbali na washiriki wote wa jukwaa hilo kwa ujumla.

Rais Dk. Mwinyi alipata fursa ya kutembelea maonesho ya biashara ndani ya Hoteli ya Mulia kutoka nchi washiriki wa Jukwaa la Indonesia na Afrika 2024 ikiwamo Tanzania.

# ZRA yavuka lengo ukusanyaji mapato Agosti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA) imevuka malengo la ukusanyaji wa kodi kwa mwezi wa Agosti mwaka huu kwa kukusanya Sh. bilioni 71.1.

Kaimu Kamishna Mkuu wa ZRA, Said Ali Mohamed, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa hiyo kwa waandishi wa habari katika ofisi za ZRA Mazizini Mkoa wa Magharibi Unguja.

Alisema fedha hizo ni ufanisi wa asilimia 102.34 ya makusanyo yaliyotarajiwa kwa mwezi huo, pamoja na kuvuka malengo yaliyowekwa.

Alisema kuwa kipindi cha Agosti ZRA ilikadiriwa kukusanya Sh. bilioni 69.49, kwamba wamefanikiwa kuvuka malengo yaliowekwa na serikali.

Alisema makusanyo halisi ya Agosti mwaka uliopita wa 2023 yalikuwa Sh. bilioni 57.238 ambayo yamekuwa kwa asilimia 24.24 yakilinganishwa na makusanyo halisi ya Agosti mwaka huu.

"Tukifanya mlinganisho baina ya kiasi kilichokusanywa Agosti mwaka 2023/2024 na Agosti mwaka 2024/2025 kuna ongezeko la Sh. bilioni 13.87," alisema.

Akielezea sababu zilizopelekea kufanya vizuri alisema ni pamoja na kuimarika na kuongezeka shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, ambazo zinatokana na sera na uongozi mzuri wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan zilizoimarisha mazingira ya biashara kwa pande zote mbili.

**"Tukifanya mlinganisho baina ya kiasi kilichokusanywa Agosti mwaka 2023/2024 na Agosti mwaka 2024/2025 kuna ongezeko la Sh. bilioni 13.87," alisema.**

Sababu nyingine ni uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar, unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za serikali chini ya uongozi wa Dk.Hussein Ali Mwinyi.

Aidha, alisema utekelezaji wa marekebisho ya sheria za kodi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni hatua iliyopelekea kuimarika kwa ukusanyaji katika vianzio vya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ushuru wa bidhaa, ada za bandari na kodi ya miundombinu. "Kuimarika kwa ushirikiano baina ya wizara na taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ta Utalii na taasisi za serikali, kuimarika kwa uhusiano na ushirikiano kati ya ZRA na wafanyabiashara imechangia ukuaji mapato," alisema.

Alisema mikakati ya ukusanyaji wa kodi kwa Septemba alisema, ZRA itaendelea kuimarisha mfumo wa kusomana (ZIDRAS) kati yao na walipakodi pamoja na mifumo ya taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za walipakodi. "Hatutosita kufanya ziara ili kutambua na kutatua changamoto za wafanyabiashara na migogoro ya kikodi kwa wakati, ikiwamo kuweka mazingira ya usimamizi wa sheria za kodi yatakayoondoa changamoto za wafanyabiashara," alisema.

Akizungumzia kuhusu wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi alisema watawachukulia hatua za kisheria.



Kijana (kushoto), akiwaonesha wageni na watalii mbalimbali, kiumbe cha baharini kiitwacho ngadu chenye nguvu za ajabu, walipotembelea fukwe ya Bahari ya Hindi, katika Kisiwa cha Kwale, Fumba Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wadau Bandari ya Zanzibar walia na changamoto

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wanaotoa huduma katika Bandari ya Zanzibar wameliomba Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC), kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya changamoto zinazodumaza utoaji wa huduma katika eneo hilo, ili kuinua uchumi wa nchi.

Walitoa ombi hilo mjini Unguja katika kikao cha kuwasilisha ripoti ya utendaji kazi na kuchukua maoni ya wadau hao ili kusaidia kutengeneza mpango kazi wa shirika hilo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Juma Ali miongoni mwa wadau hao alisema licha ya kuwa takwimu zilizowasilishwa katika taarifa ya utendajikazi wa shirika hilo zinaonesha ufanisi umeongezeka lakini bado baadhi ya changamoto zinahitaji kutafutiwa ufumbuzi ili malengo yaweze kufikiwa.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na suala la meli zisizomilikiwa na wazawa kufanya kazi katika Bandari ya Zanzibar bila kufuata sheria ikiwamo kujisajili kama wawekezaji.

Alisema hali hiyo inasababisha kudorora kwa utendaji kazi wa meli za wazawa na kuikosesha serikali mapato.

Bakari Hamad alisema uzoefu unaonesha kuwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia, dunia inafanya kazi kupitia mifumo, hivyo alilitaka shirika hilo la bandari kuimarisha huduma hiyo ili kwenda sambamba na mageuzi ya kiutendaji na kuimarisha utendaji kazi wao.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Akif Ali Khamis, alisema shirika hilo litaendelea kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya changamoto ambazo bado ni kikwazo kwa wadau hao hasa suala la ongezeko la meli za kigeni ili kuwalinda wafanya biashara wa ndani.

Akitoa tathmini ya utendaji kazi wa shirika hilo toka lilipokabidhiwa kwa mwekezaji, Atif alisema taasisi hiyo imefanikiwa kuondoa changamoto mbalimbali ikiwamo ya meli kusubiri kutia nanga kutoka siku 20 au 40 hadi kufikia chini ya siku 10.

Alisema pia imefanikiwa kupunguza mrundikano wa makontena matupu katika eneo la Bwawani.

Alisema utekelezaji huo ni zaidi ya asilimia 50 ya utendaji waliokubaliana na mwekezaji huyo katika kipindi cha mwaka mmoja na kwamba changamoto iliyobakia ni ya mizigo kwa ajili ya wateja.

Alisema wanatarajia kuitumia Bandari Kavu ya Maruhubi, wakati wowote watakapopata leseni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema kuwa hatua hiyo itaongeza idadi ya mzigo inayopakuliwa kwa siku na kupunguza msongamano wa abiria katika eneo hilo na kupisha Bandari ya Malindi kuhudumiwa zaidi watalii ili kuboresha haiba ya mji.

Hata hivyo, alisema shirika hilo linawakaribisha wawekezaji wa ndani kushirikiana nao ili kuongeza kasi ya uboreshaji wa utoaji wa huduma katika eneo hilo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA CHETI



**BENIDA ROGASIAN MAPEMBE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0266-0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **REGINAMUNDI SECONDARY SCHOOL mwaka 2020**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KAG/MIS/11325/2024.**

### KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**KAMALDEEN MUCCADAM** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 149183** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2024. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/186594/2024**

### KUPOTEA KWA VYETI



**ZABLON SAMON ZACHAYO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2117-0036** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IGALUKILO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017 na CHETI CHA CHUO chenye usajili namba **E0516-0125** kilichotolewa na **MURUTUNGURU TC** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/188202/2024**

### KUPOTEA KWA CHETI




**HALID HUSSEIN LUGAIMKAMU,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S0613-0179** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2015 kupitia shule ya sekondari Nyampulukano. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/39305/2024**

### KUPOTEA KWA CHETI



**PERPETUA MVANDA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S0325-0074** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2007 Kupitia Shule ya sekondari Lugalo. Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **MT/214/VOL.VIII/98**

### KUPOTEA KWA CHETI



**DEBORA PETER LUPANDAMHULI,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index No **S1804-0014** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Kilabela Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MWA/ILE/32903/2024**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KHALFAN HASSANI LULIMI,** Anatangaza kupotea kwa Kadi ya Pikipiki aina ya haojue yenye namba za usajili **mc 222 dnq,** Chassis Namba **LC6PCK764N0001845,** ENGINE NO **157FM.1X1B03503.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/IRI/IRI/13367/2024.**

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IDDI BAKAR JUMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 829 ELM ,** CHASSIS NAMBA: **BPKM5H2T1RK010266 na ENGINE NAMBA: KL162FMJ240310266.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/32521/2024**

### CHANGE OF NAME BY DEED POLL ACT (CAP 117)

**BY THIS DEED, ALLY SALIMU HAMISI** (new name ) of ARUSHA, DO HEREBY , absolutely renounce and abandon the use of my former names **ALLY IBRAHIM SALIMU** (old name) in lieu thereof do assume the name **ALLY SALIMU HAMISI** and in pursuance of such change of my names as aforesaid.

**I ,HERE DECLARE** that I shall at all times hereafter and in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon occasions whatsoever use and sign the said name of **ALLY SALIMU HAMISI** as my name I lieu of **ALLY IBRAHIM SALIMU** the names I renounced as aforesaid.

**AND I HEREBY AUTHORISE and REQUEST** all person s to designate and address me in the name of **ALLY SALIMU HAMISI.**

**VERIFICATION:**
**I, ALLY SALIMU HAMISI** make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the OATHS and Statutory Declarations Act, Cap .117
**WITNESS WHEREOF I** have here unto subscribed the name of in on the day and in the manner hereinafter appearing:

SIGNED and DELIVERED by the said ALLY SALIMU HAMISI who is known to me Personally/introduced to me by .................. the latter being known to me personally in my presence this June 13, 2024



BEFORE ME:
NAME; ..........
SIGNATURE; ..........
ADDRESS; ..........
QUALIFICATION; COMMISSIONER FOR OATHS

### THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**IN THE DISTRICT COURT MUFINDI AT MAFINGA**

**SMALL CLAIM CASE NUMBER 12597/2024.**

**YIDA IMPORT AND EXPORT COMPANY LIMITED .....CLAIMANT**

**VS**

**MPEPWA MICRO FINANCE ..............1ST RESPONDENT**
**MAJEMBE AUCTION MART.............2ND RESPONDENT**
**ZHANG MIN....................................3RD RESPONDENT**

**To ZHANG MIN....................................................**

Whereas your attendance is required to answer of the here in above names suit.

You are hereby commanded to appear in this court on the 10th day of September 2024 at 08:30 am or soon thereafter as the case is to be heard.
Here in fall not.

Given under my hand and Seal of this Court9th august day on the 9th day of August 2024.

DISTRICT MAGISTRATE MUFINDI
RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT MUFINDI

### NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**SEPCO Debt Collector & Auctioneering Co. Ltd** kwa idhini tuliyopewa na **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa mdaiwa na mdhamini kulipa deni lao. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali walizoweka dhamana ya mkopo kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Amini Joseph Ceaser/ FAIMA General Supply Ltd | Gari T 333 DGZ Ford Ranger – ipo Tabata (SEPCO yard ) | 20/09/2024 | SEPCO Debt Collector & Auctioneering Co. Ltd |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/Mdhamini/ mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO :0715683777/0750548337**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MWANZO CHA JUMUISHI Mkoa Dodoma**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 293/2024**

**Jina Mdai EMMANUEL ANDREA BWILE NA GOODWIN ATTONEY**

**Jina la Mdaiwa THERESIA DANIEL SUMBALI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( Kanuni ya 18 ya Kanuni za Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa THERESIA DANIEL SUMBALI**
**NA VERONICA DANIEL SUMBALI**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta madai yake /yao kwamba**
**(Eleza hapa habari za Madai )**
**WANADAIWA KIASI CHA TSH 9,520,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 10 Mwezi 9 Mwaka 2024 saa 9:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 2 Mwezi 9 Mwaka 2024

HAKIMU

### IN THE DISTRICT COURT OF KYELA
**AT KYELA**

**MISC. CIVIL APPLICATION FOR EXCUTION CASE NO. 19882 OF 2024**

**DEOGRATIOUS JUSTINE MASSAWE............APPLICANT**

**VERSUS**

**BACKBONE TANZANIA COMPANY...........RESPONDENT**

**TO: BACKBONE TANZANIA COMPANY OF KYELA.**

**TAKE NOTICE** that hearing of the above suit has been set down for hearing on 17th day of September 2024 at 08:30 a.m in forenoon thereafter at the District Court.

You must produce on that day all the witnesses upon whose evidence and all the document upon which you intend really in support of your case.

Given under my hand and seal of this court this 04th day of September, 2024.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I/C
KYELA

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa, Tupigie, 0677 020701*

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yaifungulia mashtaka Hamas

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imemfungulia mashtaka kiongozi wa kundi la Hamas Yahya Sinwar na watu wengine kadhaa wakituhumiwa kuhusika na shambulio la Oktoba 7, mwaka jana.

Wizara ya sheria ya nchi hiyo, ilisema inawafungulia mashtaka wanachama sita wa Hamas kwa makosa saba, ikiwamo mauaji ya raia wa Marekani, kula njama za kufadhili ugaidi na matumizi ya silaha za maangamizi.

Mashtaka hayo ya jinai yanatokana na miongo kadhaa ya madai ya kufanyika kwa mashambulizi ya Hamas, pamoja na shambulio la kihistoria lilotokea kusini mwa Israel mwaka uliopita.

Hatua hiyo ni ya kwanza kwa vyombo vya sheria vya Marekani kuwawajibisha viongozi wa Hamas katika shambulio la Oktoba 7, ingawa watatu kati yao wamekufa.

Sinwar anaaminika kujificha kwenye vichuguu katika eneo moja la Ukanda wa Gaza.

Katika taarifa yake ya video iliyotolewa Jumanne, washtakiwa walihusika na kufadhili na kuongoza operesheni ya miongo kadhaa ya mauaji ya raia wa Marekani na kuhatarisha usalama wa Marekani kutoka kundi hilo watafikishwa mahakamani.

Ilibainisha kwamba shambulio hilo dhidi ya Israeli liliua familia nzima katika mauaji yaliyoelezwa mabaya zaidi ya Wayahudi tangu mauaji ya Holocaust.

„Waliwaua wazee na kuwaua watoto wadogo. Walitekeleza unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake, ikiwa ni pamoja na ubakaji na ukeketaji.“ ilisema taarifa hiyo

Viongozi wengine wa Hamas walioshtakiwa ni pamoja na kiongozi wa zamani Ismail Haniyeh; Marwan Issa, naibu kiongozi wa mrengo wa kivita; Khaled Mashaal, ambaye anaongoza kundi nje ya Gaza na Ukingo wa Magharibi; pamoja na Mohammed Deif na Ali Baraka.

***BBC***



Kiongozi wa upinzani nchini Uganda, Bobi Wine. Akiwa amelazwa hospitali baada ya kushambuliwa na Askari polisi juzi.**PICHA: REUTERS**

# Bobi Wine aendelea vizuri

**KAMPALA, Uganda**

KiONGOZI wa upinzani nchini Uganda, Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine ambaye amejeruhiwa kwa kupigwa na pomu la kutoa machozi na polisi, imeelezwa anaendelea kupata nafuu.

Kyagulanyi alipelekwa hospitali kwa ajili ya kupatiwa matibabu baada ya bomu hilo kumjeruhi mguuni juzi.

Ni katika makabiliano na polisi, lakini chama chake

Chama cha (NUP) kinachoongozwa na Kyagulanyi, kilisema kuwa mwanasiasa huyo ambaye pia ni nyota wa pop alipigwa na bomu la kutoa machozi na sio risasi kama ilivyofikiriwa mwanzoni.

Tukio hilo lilitokea wakati kiongozi huyo akiwa njiani kwenda kuwatembelea mawakili wake katika eneo la Bulindo, kilomita 20 kaskazini mwa mji mkuu wa Kampala.

Taarifa iliyotolewa na polisi ilisema kiongozi huyo wa upinzani alijikwaa wakati akiingia kwenye gari lake.

Awali, akaunti ya mtandao wa X ya Bobi Wine, ilichapisha taarifa hiyo kwa mara ya kwanza, akisema amepigwa risasi mguuni na polisi huko Bulindo.

Kanda za video zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii na mwanahabari Solomon Serwanjja, ambaye alikuwa katika eneo la tukio, ikimwonesha kiongozi huyo akisaidiwa kutoka kwenye jengo akiwa na jeraha katika paja lake la kushoto ambalo lilitoa damu.

Madaktari wa Hospitali ya Nsambya iliyoko Kampala waliambia BBC kuwa kiongozi huyo wa NUP anatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa kuondoa vipande vya bomu la kutoa machozi wakati wowote.

Wakati huo huo, Tume ya Haki za Binadamu ya Uganda (UHRC), imetaka kuachiliwa huru kwa wanawake watatu waliokamatwa na kuwekwa rumande kwa makosa ya kufanya maandamano nje ya Bunge wakiwa nusu utupu.

Kiongozi wa tume hiyo, Mariam Wangadya, wakati akizungumza na Monitor, alilaani hatua zilizochukuliwa dhidi ya wanawake hao.

Alisema kukamatwa kwao ni ukiukwaji wa haki zao za msingi.

Wanawake hao Norah Kobusingye, Praise Aloikin Opolose, na Kemitooma Kyanzibo wako rumande tika Gereza la Luziratangu Jumatatu kwa madai ya kuleta usumbufu kufuatia maandamano yao ya kupinga ufisadi.

“Waliokuwa wamejizatiti walikuwa na mabango. Bunge ni mahali ambapo viongozi wao wote waliowachagua wanakaa. Norah, Praise na Kemitooma walikuwa na kila haki ya kutembea hadi Bungeni kudai kusikilizwa. Hazikuwa na madhara yoyote kwa umma au kwa mtu yeyote,” Bi Wangadya alisema.

„Polisi walichopaswa kufanya ni kuandamana nao hadi Bungeni ambako wangekutana na Spika wao au mwakilishi wake ambaye angewasikiliza na kupokea maombi yao na sio kuwakamata,” alisema wangadya.

***BBC***

# China kuboresha reli ya Tazara

**BEIJING, China**

MARAIS wa China, Tanzania na Zambia wametia saini mkataba wa makubaliano kuhusu kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli na bahari.

Viongozi hao, Xi-Jinping wa China, Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Hakainde Hichilema wa Zambia, walikutana nchini China ambako kunafanyika mkutano wa nchi za Kiafrika na taifa hilo lenye uchumi mkubwa duniani.

Shirika la habari la China, limeripoti jana nchi hizo tatu zimesaini makubaliano hayo ya mwanzo kuhusu mradi wa reli unaolenga kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli na bahari katika kanda ya Afrika Mashariki.

Marais Xi-Jinping, Samia Suluhu Hassan na Hakainde Hichilema ni miongoni mwa viongozi wanaoshiriki mkutano wa ushirikiano kati ya China na Afrika ulioanza rasmi jana.

Shirika hilo la habari la China limesema, nchi hiyo iko tayari kuutazama mkutano huo kama fursa ya kupiga hatua mpya ya kufufua ushirikiano wa reli kati ya Tanzania na Zambia ili kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli na bahari kwenye kanda hiyo.

Mwanzoni mwa mwaka huu Benki ya Dunia iliidhinisha dola milioni 270 za kusaidia kuimarisha usafiri wa reli kati ya mataifa hayo jirani ya Tanzania na Zambia katika kunyanyua biashara kwenye eneo hilo.

***DW***

**Shirika hilo la habari la China limesema, nchi hiyo iko tayari kuutazama mkutano huo kama fursa ya kupiga hatua mpya ya kufufua ushirikiano wa reli kati ya Tanzania na Zambia ili kuimarisha mtandao wa usafiri wa reli na bahari kwenye kanda hiyo.**

# KVZ kamili yaifuata Mwenge FC Pemba

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha KVZ FC kimeondoka Unguja na kuelekea Pemba kwa ajili ya mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Zanzibar dhidi ya wenyeji Mwenge itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Gombani, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa KVZ, Abdul-Jalili Mohamed, alisema timu hiyo imeondoka na msafara wa wachezaji 23 wakati nyota wake wawili wameitwa kujiunga na kikosi cha Timu ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngongororo Heroes).

Mohamed alisema wamejiandaa vizuri kupata ushindi katika mchezo huo na walitumia mapumziko mafupi kurekebisha mapungufu waliyoyabaini katika kikosi chao kwenye mazoezi ya mwisho.

“Tumeamua kwenda mapema tofauti na ilivyozoeleka huko nyuma timu husafiri siku moja kabla ya mchezo, tumefanya hivi ili wachezaji wapate muda wa kupumzika ili kujiandaa vyema na mchezo, tunautaka mchezo,“ alisema Mohamed.

Aliongeza watacheza kwa tahadhari kwa sababu wanajua wenyeji pia wamejipanga kuzibakisha pointi nyumbani hivyo mashabiki watarajie mechi yenye viwango vya juu.

Alisema licha ya wapinzani wao kupanda daraja msimu huu, hawatawadharau na wataingia dimbani kwa kuwapa heshima.

“Kila timu inataka kufanya vizuri katika mchezo wake wa kwanza, hivyo huu mchezo ni mgumu na unachukuliwa kwa uzito, kwa sababu kila mmoja anataka atimize lengo lake,“ alisema.

Aliwataka mashabiki wa timu hiyo walioko Pemba kujitokeza kwa wingi kuwashangilia ili kuongeza hamasa kwa wachezaji wao.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajia kuanza rasmi kesho kwa mabingwa watetezi, JKU kuwavaa Inter Zanzibar iliyopanda daraja, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Amaan Complex.

Ligi hiyo itaendelea tena keshokutwa kwa Mlandege kuwakabili Chipukizi FC huku Septembe 8, mwaka huu ,Wanagenzi Mwembe‘ Makumbi City wataikaribisha New City huku Tekeleza FC wao wataanza msimu mpya kwa kuwakabili Kipanga FC huku Septemba 9, mwaka huu Mafunzo itacheza dhidi ya KMKM.

# IBENGE, LYOGOPE WATAJWA KUPOKEA MIKOBA YA DABO

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuachana na Youssouph Dabo, ambaye ni raia wa Senegal, uongozi wa Azam FC unatarajia kumtangaza rasmi kocha wake mpya kesho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema wako katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kupata kocha ambaye atakuja kukinoa kikosi chao.

Ibwe alisema kwa sasa timu yao inaongozwa na benchi la ufundi wa timu ya vijana.

Ofisa huyo alisema katika mchakato huo hadi jana wamebakia makocha wanne na mmoja wao ndio atapewa jukumu la kuiongoza timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Tuko katika mchakato wa kusaka mwalimu, ulianza siku mbili nyuma kabla ya kutangaza kuachana na Kocha Dabo, kulikuwa na makocha wengi waliomba kurithi mikoba yake, lakini katika mchujo wa makocha wanne ambao wamesajiliwa na tutamtangaza siku mbili hizi, kipindi hiki hiki cha mapumziko ya kalenda ya FIFA,“ alisema Ibwe.

Akitoa sababu ya kumwonyesha mlango wa kutokea Dabo, alisema uamuzi umefikiwa baada ya kuona mashabiki wengi hawafurahishwi na jinsi timu ilivyocheza michezo minne iliyopita kuanzia dhidi ya Yanga kwenye Ngao ya Jamii pamoja na mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya APR ya Rwanda, na mmoja wa Ligi Kuu dhidi ya JKT Tanzania,“ alisema.

Hata hivyo, alisema si Dabo ni kocha mbaya kwa sababu ni yeye ndiye kwa mara ya kwanza baada ya misimu 10, amewarejesha kucheza mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

“Wakati mwingine tu upepo unakataa, lakini tunamshukuru yeye na mwenzake Bruno Ferry kwa kutufikisha hapa tulipofika,“ aliongeza Ibwe.

Aliyekuwa Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Lyogope, anatajwa kutua katika benchi la ufundi la timu hiyo yenye makazi yake Chamazi.

“Ni kweli Lyogope atakuwa mmoja kati ya makocha watakaohudumu benchi la ufundi la Azam, tusubiri mabosi watakapotangaza rasmi ujio wake,“ chanzo chetu kilisema.



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itarejea tena baada ya kumalizika kwa Kalenda ya Kimataifa ya FIFA. **PICHA: MTANDAO**

# Edna ‘kuibeba’ Yanga Princess

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache baada ya kurejeshwa, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema atakibadilisha kikosi hicho na kuwa timu yenye ushindani kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Lema ambaye ameanza ,pre season‘ na kikosi hicho juzi, aliliambia gazeti hili lengo lake ni kuirudisha Yanga Princess ambayo wengi waliizoea ya kucheza mpira mzuri na wenye ushindani.

Alisema Yanga Princess haikuwa timu yenye ushindani katika misimu ya hivi karibuni na sasa anajipanga kurejesha makali yake.

“Nashukuru, nimefurahi kurejea tena hapa, maana ndiyo sehemu ambayo nilianza maisha yangu ya ukocha, nimerejea tena kwa wakati mwingine, tunahitaji kutengeneza timu nzuri, unaweza kuwa na wachezaji wengi wazuri lakini ukawa huna timu.

Tunataka kuirudisha Yanga Princess ambayo wengi waliizoea, ile inayocheza vizuri na kupata matokeo mazuri, najua haitakuwa rahisi lakini kwa sababu ndiyo kazi yetu tunapaswa kufanya hivyo, kuhakikisha timu inarejea kwenye uimara wake, tunawaambia wanachama na mashabiki wa Yanga wawe na subira na watusapoti,“ alisema Lema.

Alisema ana kazi ya ,ziada‘ ya kufanya kwa sababu ya kusajili wachezaji wengi wapya kutokana na nyota waliokuwapo msimu uliopita kuondoka.

“Tuna wachezaji wengi wapya, zaidi ya 10, sasa hivi tumesajili wachezaji kutoka nje na ndani ya nchi, kwa sasa tunaangalia kwanza wana nini na wanaweza kutupa kitu gani ili kuandaa programu vizuri,“ Lema alisema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO ATAKIWA UTURUKI

KLABU ya Galatasaray wapo kwenye mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa mkopo wa mwaka mmoja kwa kiungo wao wa kati wa Brazil, Casemiro, mwenye umri wa miaka 32. ***(Ali Naci Kucuk)***

### SALAH, LIVERPOOL KUTETA

LIVERPOOL inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 32, baada yeye kusema huu unaweza kuwa msimu wake wa mwisho. ***(Football Insider)***

### HUERTA ALITAJWA LIVERPOOL

KOCHA wa Pumas UNAM, Gustavo Lema, amesema Liverpool ilijaribu kumsajili winga wao wa kimataifa wa Mexico, Cesar Huerta, mwenye umri wa miaka 23. ***(TUDN}***

### CHELSEA KUMTOA CHILWELL

KLABU ya Chelsea wako tayari kumpeleka beki wa kushoto wa England, Ben Chilwell, mwenye umri wa miaka 27 kwa mkopo nchini Uturuki, ingawa bado hawajapokea ofa yoyote. ***(Telegraph)***

### FOFANA ATAKIWA UGIRIKI

MAZUNGUMZO yanaendelea kati ya Chelsea na AEK Athens ya Ugiriki kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, David Datro Fofana, mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### CARDOSO ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imefanya mazungumzo ya kumnunua kiungo wa kati wa Marekani, Johnny Cardoso, mwenye umri wa miaka 22 kwa dau la pauni milioni 21 kutoka Real Betis. ***(Telegraph)***

### KEITA KUTUA ISTANBUL

KIUNGO wa kati wa zamani wa Liverpool, Naby Keita, mwenye umri wa miaka 29, yuko kwenye mazungumzo na klabu ya Istanbul Basaksehir kuhusu uwezekano wa kuhamia huko. ***(Guardian)***

### MARTIAL MSHAHARA JUU

WINGA wa zamani wa Manchester United, Anthony Martial, mwenye umri wa miaka 28, amepewa mkataba na AEK Athens ambao utamfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kuwa ndiye anayelipwa fedha nyingi zaidi klabuni hapo. ***(Sport24 via Sun)***

### UNITED YAMTAKA CABAL

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa kushoto wa Juventus mwenye umri wa miaka 23 ambaye ni raia wa Colombia, Juan Cabal. ***(Tutto Juve)***

### ERIKSEN AKARIBIA BETIS

KLABU ya Real Betis ilitoa ofa kwa kiungo wa kati wa Manchester United na Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 32, siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho. ***(Fabrizio Romano)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE BRUYNE: SIJAWAZA KWENDA SAUDI ARABIA

Mshambuliaji huyo asema hajawahi pia kufanya mazungumzo na...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin De Bruyne amesema hakuwa na mawasiliano yoyote na klabu yoyote kuhusu kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England msimu huu wa joto.

Mbelgiji huyo Juni alikiri angefikiria uhamisho wa kwenda Saudi Pro League, ambao hapo awali walikuwa wamemteua kama shabaha kuu kwa miaka ijayo.

Hata hivyo, Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, baadaye alifafanua De Bruyne hataenda popote wakati timu yake ikijaribu kushinda taji la tano la ligi msimu huu.

Sasa, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amefichua hakuwasiliana na wanunuzi wowote na kwa sasa akili yake yote ipo uwanjani.

Aliiambia BBC Radio Manchester: "Sijazungumza na mtu yeyote, kusema ukweli.

"Kumekuwa na kelele na habari nyingi, nilisema wakati wa kiangazi natarajia majira ya joto na ndicho kilichotokea, nimekuwa likizo kwa wiki nne, nikarudi na kuanza mazoezi. Ilikuwa hivyo. Hakuna cha kusema."

De Bruyne anaingia msimu wake wa 10 kama mchezaji wa Manchester City na mkataba wake wa sasa utakamilika mwishoni mwa kampeni, ingawa anatarajia mazungumzo ya kuongeza muda yataanza hivi karibuni.

Aliongeza: „Siwasiliani na mtu yeyote au kuzungumza na mtu yeyote.

„Mara tu msimu unapoendelea, nina uhakika kutakuwa na mazungumzo na City.

"Nataka tu kujisikia vizuri, kucheza soka nzuri na hii itakuja katika miezi ijayo. Sijisikii haraka sana kwa sasa."

De Bruyne alirudishwa kwenye kikosi cha City baada ya Euro 2024, akitokea kwenye Ngao ya Jamii kama mchezaji wa akiba aliyechelewa, lakini ameanza ushindi wao mara tatu wa Ligi Kuu, akifunga na kusaidia katika ushindi wa 4-1 dhidi ya Ipswich Town.

Atakuwa nahodha wa Ubelgiji wakati wa mapumziko ya kimataifa ya Septemba kwa mechi mbili za Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Israeli na Ufaransa.

HABARI MICHEZO

# WATATU WAJIONDOA KIKOSI CHA ENGLAND

**LONDON,** England

ENGLAND imethibitisha Phil Foden, Cole Palmer na Ollie Watkins wote wamejiondoa katika kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya mapumziko ya kimataifa ya Septemba hii.

Foden alikuwa na shaka inayojulikana kuelekea mechi za Ligi ya Mataifa ya Uefa, baada ya kukaa nje ya mechi mbili za mwisho za Manchester City, Kocha wake, Pep Guardiola alikiri asingeweza kuicheza England.

Kiungo huyo wa kati hata hakuripoti kikosini kwa sababu ya ugonjwa wake na sasa ameondolewa rasmi kwenye kikosi pamoja na Palmer na Watkins.

"Kikosi cha Simba Watatu kiliripoti kwenye Uwanja wa St. George's Park Jumanne, lakini baada ya tathmini wote wawili Palmer na Watkins walirejea katika klabu zao," ilieleza taarifa fupi ya timu ya taifa ya England.

Muhimu kwa Chelsea na Aston Villa, sio Palmer wala Watkins anayeaminika amepata majeraha yoyote zaidi.

Palmer alionekana kuumia msuli wa paja wakati wa mechi ya kufuzu Ligi ya Europa Conference dhidi ya Servette, lakini alikamilisha dakika 90 dhidi ya Crystal Palace siku tatu baadaye. Chelsea ilithibitisha kujiondoa kwake.

Kwa upande wa Watkins, mshambuliaji huyo ameondolewa katika muda wa saa katika kila mechi kati ya mechi tatu za Ligi Kuu England za Villa, huku kocha, Unai Emery akisisitiza hana utimamu wa kutosha baada ya muda mrefu wa kiangazi akiwa na England kwenye michuano ya Euro 2024.

"Alikuwa anakuja hapa akiwa na jeraha dogo, kwa kweli hakuwa fiti kwa asilimia 100 alipoanza mazoezi nasi," alisema Emery.

"Alihitaji muda wa mapumziko wa wiki moja zaidi kuliko wachezaji wengine baada ya kurejea."



# United yaeleza sababu kumtoa Sancho

**LONDON,** England

MKURUGENZI wa Michezo wa Manchester United, Dan Ashworth, amefichua klabu hiyo ilimruhusu, Jadon Sancho, kujiunga na Chelsea kwa sababu walikuwa na wachezaji wa kutosha katika nafasi yake.

Sancho alijiunga na The Blues hao kwa mkopo akiwa kipengele cha kununuliwa mwishoni mwa msimu, na hivyo kuzima hali ya kutofanikiwa kwa miaka mitatu Old Trafford.

Winga huyo alikaribishwa tena katika kikosi cha kwanza cha United wakati wa maandalizi ya msimu mpya baada ya kugombana na Kocha, Erik ten Hag.

Wakati wa mahojiano mapana na waandishi wa habari wa Uingereza pamoja na Mkurugenzi Mtendaji, Omar Berrada, Ashworth alieleza kwa nini United ilimwachilia Sancho.

"Kuhama na kwenda kwa klabu mpya na ni sawa kwao na ni sawa kwetu, basi unapaswa kuchunguza. Tulihisi tuna kina cha kutosha katika nafasi yake.

"Tuna wachezaji wanne wazuri wa upana, Jadon alikuwa wa tano, na ilituwezesha kufanya uamuzi huo, kama ulikuwa mzuri kwake na mzuri kwetu, lilikuwa jambo ambalo tulikuwa tayari kuzingatia."

Alipoulizwa kama Sancho hana mustakabali ndani ya United, Ashworth alijibu: "Hakuna cha kufanya na hilo. Ulikuwa uamuzi ambao tulifanya - ikiwa ni sawa kwa Jadon na ni sawa kwetu kusonga mbele.

"Alitaka kuchunguza nafasi hiyo akiwa Chelsea, kama Scott alitaka kutafuta nafasi huko Napoli, kama vile Aaron alitaka kutafuta nafasi huko West Ham."




# Pochettino kizungumkuti Marekani

**MIAMI,** Marekani

BEKI wa Marekani, Tim Ream, amesema wachezaji hawajafahamishwa kuhusu uteuzi unaokuja wa Mauricio Pochettino kama kocha mkuu wa timu hiyo.

"Tunajua kama kila mtu mwingine," alisema Ream, akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari.

"Tuliambiwa wiki chache zilizopita utafutaji ulikuwa ukienda kwa mwelekeo mzuri na kwa wakati huu ndipo kila mtu yuko.

"Tunajisikia na tumeambiwa jambo linapotokea, tutajua. Na kila mtu atajua haraka sana. Kwa hiyo tunasubirishwa, lakini hatujaambiwa chochote hadi sasa."

Ingawa vyanzo vilithibitisha kwa ESPN Pochettino alikubali kuwa kocha wa Marekani Agosti, mkataba bado haujakamilika.

Pochettino lazima kwanza asuluhishe suala la kimkataba na mwajiri wa zamani Chelsea, ikizingatiwa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England inamdai fedha baada ya kuachana naye mwishoni mwa msimu uliopita.

Vyanzo viliiambia ESPN mapema wiki hii mazungumzo kati ya Chelsea na Marekani yalikuwa karibu kukamilika.

Kwa sasa Marekani itasimamiwa na Mikey Varas kwa muda kwa kipindi cha dirisha la Septemba, timu hiyo ikimenyana na Canada na New Zealand katika mechi mbili za kirafiki.

Ream, ambaye alikumbana na timu zinazofundishwa na Pochettino alipokuwa akiichezea Fulham, alimwita kocha huyo wa Argentina "wa kiwango cha juu."

"Timu zake huwa ngumu kucheza dhidi yake," alisema Ream, ambaye hivi karibuni alijiunga na Charlotte FC ya MLS kutoka Fulham.

"Ni wazi, ni kocha wa hali ya juu, wa kiwango cha juu. Ni timu zilizojipanga vizuri na zenye nguvu katika ushambuliaji.

"Kwa hiyo, kila mara ni ngumu kucheza dhidi yao na sidhani kama nilikuwa kwenye mwisho sahihi wa mechi yoyote ambayo nilicheza dhidi yao."

Beki huyo baadaye aliongeza kuwa mabadiliko ya kocha yanapaswa kufanya kazi ili „kuinua nguvu na umakini" wakati timu inapoanza maandalizi ya Kombe la Dunia la 2026.

Marekani inarejea uwanjani kwa mara ya kwanza tangu ilipotolewa raundi ya mtoano ya 2024 Copa América, baada ya kushinda mchezo mmoja tu wa kundi. Kocha, Gregg Berhalter alifutwa kazi baada ya Copa America.

HABARI MICHEZO

# SERENGETI GIRLS MAJARIBUNI MOROCCO MICHUANO UNAF

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), inatarajia kukutana na yosso wenzao wa Morocco katika mechi ya mashindano ya UNAF itakayochezwa leo jijini Tunis nchini, Tunisia.

Serengeti Girls ambayo ni nchi mwalikwa katika mashindano hayo ilianza kwa ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Misri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime, alianza kwa kuwapongeza wachezaji wake kwa kiwango kizuri walichokionesha kwenye mechi ya kwanza na anatarajia wataendelea kuimarika.

Shime alisema ameendelea kukijenga kikosi chake kwa sababu malengo yake ni kurejea nyumbani na ubingwa wa mashindano hayo.

Kocha huyo alisema mashindano hayo ni muhimu na yanawasaidia wachezaji wake kujijenga kisaikolojia na kuwapa uzoefu wa michezo ya kimataifa.

"Ninawapongeza sana wachezaji wangu kwa kiwango walichokionyesha katika mchezo wetu dhidi ya Egypt (Misri), haya mashindano ya UNAF ni makubwa na yanasaidia kuwajenga wachezaji wetu ambao wengi ni chipukizi na tunatumia kuwaandaa na michuano mingine iliyoko mbele yetu,“ alisema Shime.

Aliongeza siri ya kupata ushindi mnono katika mechi ya kwanza ni wachezaji wake kufuata maelekezo na kuwakumbusha kuwa watulivu wanapokaribia goli la wapinzani.

"Ingawa hatujapata muda mrefu wa kufanya maandalizi kwa ajili ya kushiriki mashindano haya, tunashukuru tumeanza vizuri, wachezaji wamecheza wakati wa jua kali, nyasi zilikuwa zinachoma lakini wamepambana na kupata magoli manne,“ alisema Shime.

Kocha huyo pia aliwashukuru Watanzania waliopo Tunisia kwa ushirikiano waliowaonyesha katika mchezo huo kwa kujitokeza uwanjani kuishangilia timu yao.

Serengeti Girls itashuka tena dimbani kesho kuvaana na wenyeji Tunisia.



Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Athumani Nyamlani (kulia), akibadilishana mawazo na makocha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars). Kushoto ni Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Morocco, Jamhuri Kihwelo ‚Julio‘ (katikati) na Juma Mgunda baada ya mazoezi ya mwisho ya kujiandaa kuivaa Ethiopia hapo jana jioni. **PICHA: TFF**

# Mashujaa yaipigia hesabu Pamba

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Mashujaa FC kimeweka kambi Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba Jiji utakaochezwa Septemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohammed Abdallah ‚Bares‘ amesema baada ya mapumziko ya wiki moja, timu yake imeanza mazoezi ili kujiimarisha kuelekea mchezo huo utakaokuwa na upinzani.

Bares alisema licha ya kutopoteza mechi, anarejea kwenye uwanja wa mazoezi kuimarisha sehemu ambazo amebaini zinahitaji kuboreshwa.

„Tulipata mapumziko ya wiki moja, sasa tunarejea kambini kujiandaa na mchezo mwingine wa Ligi Kuu, tumecheza mechi mbili mpaka sasa, kuna mazuri yapo, lakini pia kuna mapungufu nimeyaona, nakwenda kuyarekebisha,“ alisema kocha huyo.

Mashujaa ilianza msimu mpya Agosti 17, mwaka huu kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, shukrani kwa straika wa zamani wa Yanga, Crispin Ngushi kufunga huku Agosti 23, mwaka huu ililazimishwa suluhu na Maafande wa Prisons.

## Mzize : Mimi ni hatari zaidi nikianzia benchi

INATOKA UK. 24

namshukuru Mungu, maana unaweza kuanzia nje na usifanye vizuri na ukaanza pia usifanye kile kinachotakiwa.

Ila niseme tu ukiwa nje na wenzako wanacheza ndani kwangu mimi nakuwa na uwezo wa kuusoma mchezo vizuri, udhaifu wa wapinzani na safu ya ulinzi, unaona ukikaa pale, ukifanya hivi, basi utafanya kitu tofauti na kuisaidia timu,“ Mzize aliongeza.

Nyota huyo alisema pia ingawa mguu wake wa asili anaotegemea katika soka ni wa kulia, lakini mguu wa kushoto ndiyo ina nguvu zaidi ya kupiga mashuti, kukokota mpira na kutoa pasi kuliko wa kulia.

"Mimi mguu wangu ni wa kulia, lakini mguu wa kushoto unakuwa na nguvu zaidi kwa kutoa pasi na kukokota mpira na uko vizuri kufanya hivyo kuliko wa kulia na hiki kitu hakikuja kwa bahati mbaya, nimejifunza na nimefanya hivyo kwa kuwaangalia wachezaji wa nje akiwamo Cristiano Ronaldo, yule jamaa mguu wake wa kulia, lakini akipiga kushoto kama kulia.

Kwa sasa akitaka kuwa mchezaji bora ni lazima uwe una uwezo wa kutumia mguu yote miwili, hata kama haitokuwa na nguvu sawa, lakini ikaribiane,“ aliongeza mchezaji huyo.

Katika msimu mpya ulioanza, Mzize amecheza mechi sita, mbili akianza na nne akitokea benchi ambapo mara nyingi anafunga na kuwa hatari kwa mabeki, amesema huwa hakai benchi tu na kuangalia soka, bali anakuwa na kazi ya kocha ya kuusoma mchezo, kujua timu pinzani ina mapungufu wapi, hasa eneo ya mabeki.

Timu nyingine ambazo zimeonyesha nia ya kutaka huduma ya Mzize ni Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Aalborg BK ya Denmark na Crawley Town FC inayocheza Ligi Daraja la Pili nchini Uingereza.

Mchezaji huyo alifunga bao la pili katika mechi ya kwanza ya msimu ya Yanga iliyomaliza kwa ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, goli la kwanza likipachikwa na Mkongomani Maxi Nzengeli.

Yanga pia imesonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuiondoa Vital'O ya Burundi kwa kuwafunga mabao 10-0 na sasa hatua inayofuata itakutana na mabingwa wa Ligi Kuu Ethiopia, CBE.

## Simba yajiimarisha ‘kuwaliza’ Walibya

INATOKA UK. 24

"Tunaendelea na maandalizi ya safari, tunatarajia kuondoka kati ya Septemba 12 au 13, hii itategemea na upatikanaji wa ndege, nchi ile kuunganisha ndege kuna changamoto kiasi fulani,“ alisema Rweyemamu.

Katika hatua nyingine, mechi kati ya Azam FC dhidi ya Simba imepangwa kufanyika Septemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Awali mechi hiyo ilikuwa haijapangiwa siku kutokana na kutotaka kugongana na Kalenda ya Kimataifa ya FIFA.

Michezo

Alhamisi Septemba 5, 2024
Nipashe

## De Bruyne: Sijawaza kwenda Saudi Arabia

UKURASA 21



# Mzize : Mimi ni hatari zaidi nikianzia benchi

### Afunguka mguu wake wa kushoto una nguvu sawa huku akiwa...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Clement Mzize, amesema yeye ni hatari zaidi akitokea benchi kuliko akianza katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo inayofundishwa na Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Mzize ambaye yuko katika rada za Wydad Casablanca ya Morocco na timu nyingine mbalimbali, aliliambia Nipashe ana kipaji cha kuusoma mchezo na makosa ya wapinzani kabla ya kwenda kuyafanyia kazi na ndio sababu amekuwa akifanya vizuri anapotokea benchi.

Alisema amekuwa na uwezo mzuri wa kwenda kurekebisha makosa ya wenzake na kuongeza nguvu pale panapohitajika na sababu hiyo anafurahia zaidi kuanzia benchi badala ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza.

"Kama mnavyoona mimi nikiingia kipindi cha pili ninakuwa moto kwa sababu kuna kitu nakuwa nimekisoma, walinzi wa timu pinzani wana makosa fulani wanayafanya, nikiingia nakufanyia kazi na nyinyi wenyewe mnaona huwa kinatoa majibu mazuri," alisema Mzize.

Aliongeza si kwamba yeye anaomba awekwe benchi ili aingie kipindi cha pili na kufanya hivyo, bali ni mipango ya Gamondi, ambaye huenda tayari ameshaona akiingia anampa matokeo chanya katika kikosi chake.

„Kutokea benchi ni mipango wa mwalimu, anaweza kukupa mechi moja uanze, nyingine ukae nje kwanza, ila mimi

INAENDELEA UK. 23



Mzize

## Simba yajiimarisha 'kuwaliza' Walibya

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kiungo wake, Fabrice Ngoma, akirejea nchini kuungana na wachezaji wenzake, uongozi wa Simba umesema unaendelea na mikakati ili kuhakikisha wanaiondoa Al Ahly Tripoli ya Libya katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikikisho Afrika, imeelezwa.

Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini kati ya Septemba 12 au 13, mwaka huu kuelekea Libya tayari kwa mchezo huo ambao sasa utachezwa Septemba 15, mwaka huu.

Awali mchezo huo ulipangwa kufanyika Septemba 14, mwaka lakini sasa umesogezwa mbele kwa siku moja.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema viongozi pamoja na benchi la ufundi wanaendelea na mikakati kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi zote mbili za michuano hiyo.

Ahmed alisema wameshawafahamu wapinzani wao na kwa sababu hiyo wanafahamu watakavyoingia uwanjani kuwakabili.

"Benchi la ufundi linaendelea na miakakati ya kiufundi kuhakikisha tunafanya vizuri, lakini pia viongozi kwa nafasi yao nao wanaendelea na mipango kuhakikisha timu inasonga mbele," alisema Ahmed.

Aliongeza uongozi umejipanga kuhakikisha kila kitu ambacho benchi la ufundi wanakihitaji kuelekea katika michezo hiyo miwili kinapatikana ili timu hiyo ifanye vizuri na kusonga mbele.

Alisema ili kujiweka katika nafasi salama na kufikia malengo, Kocha Mkuu, Davids Fadlu, ameomba kupatiwa mechi nyingine ya kirafiki na tayari maombi hayo yamefanyiwa kazi.

"Mara baada ya mchezo wa kirafiki wiki iliyopita dhidi ya Al Hilal, Kocha Fadlu alisema anaomba kupata mchezo mwingine wa hiyo ya kirafiki kuelekea kwenye mchezo wa klabu bingwa Afrika inamaana kubwa kwake katika kukiandaa kikosi.

Wakati huo huo, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, amesema maandalizi ya safari ya kuelekea Libya katika hatua za mwisho.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >